# *Nenda, Kamwamshe Yesu*

Hebu tuendelee kusimama kwa dakika chache sasa, na tunaenda kuomba.

2 Ninataka kusema, ni majaliwa makubwa kabisa kwangu kuwa hapa usiku wa leo katika hili Grantway Assembly, na kukutana na mchungaji wenu mpendwa hapa kwenye jukwaa lake, na ushirika huu mzuri. Nilikuwa nikizifurahia hizo nyimbo, nikisimama huko nyuma, na kuwasikia hao wasichana, ninaamini ilikuwa, wakiimba hizo nyimbo nzuri za kikanisa. Na hakuna kitu kama kuja pamoja na kumtumikia Bwana, sivyo?

3 Sasa hebu tuinamishe vichwa vyetu kwa dakika moja na kuzungumza na Huyu Ambaye tumekuja kumwabudu.

4 Baba yetu wa Mbinguni, sisi ni watu wenye majaliwa usiku wa leo, kuwa hai na kukutanika hapa kukuabudu Wewe, na tunakushukuru Wewe kwa hili. Na sasa, tumekuja si kwa kusudi lolote jingine ila kukuabudu Wewe, na kukupa Wewe utukufu na sifa kwa ajili ya kile Wewe umetufanyia sisi. Na kwa hakika tunakubali kutostahili kwetu. Hatustahili hayo.

5 Na kuona siku ambayo tunaishi, wakati nuru zinafifia! Na tunahitaji leo hii kuinuka kwa nabii, kama ilivyokuwa katika siku za Samueli, wakati Eli, wakati alipoanza kufifia, na nuru zilikuwa zikizimika katika hekalu la Mungu. Ndipo Mungu akainuka jukwaani. Basi tunaomba, Bwana, kwamba utasimama jukwaani usiku wa leo miongoni mwetu, na utajionyesha Mwenyewe hai, na—nabii mkuu wa manabii wote, Mwana wa Mungu aliye hai.

6 Na sisi—sisi tunafundishwa katika Maandiko, kwamba, "Mungu katika zama za kale na katika njia mbalimbali alinena na baba zetu kupitia manabii, bali katika siku hii ya mwisho kupitia Mwana Wake Yesu Kristo." Ee, Bwana, tunaomba kwamba Wewe utakuwa miongoni mwetu usiku wa leo ku—kutujulisha Uwepo Wako, kwa kazi Zako kuu na madhihirisho.

7 Libariki kusanyiko hili, Baba, mchungaji wake, makaribisho haya ya kupendeza, mtu mwenye moyo safi, na ninii yake... na wadhamini wake wote, mashemasi, na jamii. Na jalia tu uwe ni wakati mkuu wa ushirika. Na tunatumaini kwamba tutatoka hapa tukishangilia, tukisema, "Je! mioyo yetu haikuwaka ndani yetu hapo aliponena nasi njiani?" Kwa kuwa tunaomba hayo katika Jina la Yesu, Mwana Wako. Amina.

8 Hakika inahisi vyema kuwa kanisani tena. Nilikuwa nimeenda siku chache kwenye li—li—li—likizo, kwenye ziara, ziara ya kuwinda, na kurudi. Na kujihisi mwenyewe kurudi jukwaani tena, inahisi vizuri kabisa.

9 Na sasa nilikuwa na huu mwaliko kutoka kwa mchungaji wenu hapa, Ndugu Mack, majuma fulani yaliyopita, kuja hapa chini. Lakini inatokea kwamba, mnajua, miito, na mahali pa kwenda, mpaka si—sikupata nafasi kuutimiza.

Na kesho inanibidi kuenda huko juu Phoenix.

10 Na halafu siku inayofuata tunaondoka kwenda New York kwa ajili ya ukumbi mpya ambao ndio kwanza ujengwe kule, na tunachukua siku chache za kwanza ndani yake. Na kwa hiyo tuko pamoja na Ndugu Arne Vick, na—na makanisa yanayodhamini. Na sisi ni. . .Nina hakika mchungaji wenu anamjua Ndugu Vick. Na, hapana, si Arne Vick. Samahani. Naamini ilikuwa ni John, labda ndugu, na Kanisa la Jiwe, mchungaji wa Kanisa kubwa la Jiwe, ambalo ndilo kusanyiko kubwa kuliko yote ya Kipentekoste katika New York.

11 Na ndipo tunarudi kutoka huko kurudi chini Shreveport, Louisiana, kwa ajili ya mkutano huko pamoja na Ndugu Jack Moore. Tulikuwa huko kila Shukrani. Shukrani tatu zilizopita, nilianzisha mkutano huko; Bwana alianzisha, hasa. Samahani. Na uamsho haujakoma tangu wakati huo. Kila mara, watu wanaingia, wakiokoka, na kujazwa na Roho Mtakatifu, kila mara tangu wakati huo. Na uamsho unaendelea. Na sisi tuna siku tano pamoja na wao. Na halafu ninafikiri pamoja na . . .

12 Kurudi wakati huo kwenye. . .mpaka Phoenix, kuanzia tarehe kumi na tisa, kwenye Hoteli ya Ramada kule. Kwanza, tarehe kumi na tisa, ishirini, ishirini na moja, ishirini na mbili, na ishirini na tatu, nafikiri, ni mkutano. Kwa kawaida, mimi huenda kutoka kanisa hadi kanisa, kabla ya mkutano wa Wakristo Wafanyabiashara. Lakini tuna tatizo na. . .Unaanzia kanisa la kwanza, halafu labda linalofuata ni dogo, na watu hawawezi kuingia ndani. Na kwa hiyo tunajisikia, basi, kama ningeweza kupata Ramada, ambayo huketisha pale, loo, elfu tatu au nne, vema, basi ninaweza kuwaleta wote pamoja, kila mtu pamoja, na kuendelea kwa siku nne usiku kabla ya mkutano wa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Na ninapaswa kuwa siku mbili usiku, nafikiri, nizungumze siku mbili usiku katika huo. Ambapo, Ndugu Roberts na wazungumzaji wengine hodari huzungumza kwenye mkutano huo.

13 Ndipo basi, kutoka hapo, kuenda Visalia. Na halafu tuna hadi yapata Machi, hapa katika Marekani. Ndipo basi tunaenda Ulaya kwa ajili ya ziara, hadi Juni, na wao wana kongamano la ulimwengu kule. Na halafu, pia, ninapaswa kuzungumza siku tano usiku huko Philadelphia, njiani nikirudi, pamoja na mkutano wa Kimataifa wa Wafanyabiashara wa Full Gospel. Na halafu tunaenda, kutoka hapo, kuenda Durban, Afrika Kusini, na kuendelea, kuanzia tarehe mbili Septemba hadi tarehe sita mfululizo. Na kuenda hadi Johannesburg, halafu kuenda Kenya na Nairobi, na kupitia huko.

14 Na kwa hiyo hakika sisi, ninapotangaza hili, tunahitaji maombi, kwa kuwa ninapopata uaminifu mkubwa na huruma za watu waliokutanika, hao ni Wakristo. Hizo ndizo nguvu zangu, ni katika Ukristo, na watu kuniombea. Na mimi—mimi hakika ninahitaji maombi yenu. Basi nyinyi mnifanyie hivyo, kama mtaweza.

15 Sasa, usiku wa leo, hatutaki kuchukua muda mwingi kupita kiasi, kwa sababu ni—ni—ni Jumapili usiku, na inawabidi kufanya kazi Jumatatu. Bali ninapenda tu kuzungumza kuhusu Bwana, na nitajaribu kuyafanya upesi tu iwezekanavyo. Pia ninaamini mwanangu alisema kwamba alisambaza kadi fulani za maombi kuwaombea wagonjwa, kama Bwana akiongoza kwa njia hiyo, kuwaombea watu wagonjwa.

16 Sasa, katika kuwaombea wagonjwa, sisi ni. . .Hayo ndiyo yote tuwezayo kufanya, ni kuwaombea tu wagonjwa. Kama kuna uponyaji wowote, inabidi utoke kwa Mungu. Basi sasa, kuwazia juu ya mambo hayo wakati tunapozungumza, nguvu zote unazohitaji kwa ajili ya uponyaji tayari zipo hapa, wakati Yesu Kristo Mwana wa Mungu aliponunua vitu hivi Kalvari. Na viko wazi kwa yeyote atakaye, anaweza kuwa na uponyaji wa Kiungu. Kitu cha pekee kinachohitajika kuuingiza kazini ni imani yako.

17 Wazia tu, umeme uko kwenye nyaya, lakini lazima ubonyeze kitufe. Unaona? Lazima ubonyeze kitufe. Basi kwa imani unabonyeza kitufe, ukiamini kwamba kitafanya kazi. Sasa, kama nyaya zote zimeunganishwa vizuri, na nguvu za umeme ziko katika waya, basi wakati ukibonyeza kitufe hicho jambo fulani linaenda kutukia. Vema, hivyo ndivyo ilivyo na uponyaji wa Kiungu, kwa wokovu, au sifa zote ambazo Kristo alikufa kwa ajili yake, kutupatia. Kila kitu kilimalizika Kalvari. Na jambo la pekee litupasalo kufanya, kwa imani, ni kubonyeza kitufe. Ndipo basi inaenda, hapo inawaka, unaona. Ni rahisi tu hivyo. Na hapo. . .

18 Sisi ambao huwaombea wagonjwa, mara nyingi wanatubandika jina la mponyaji wa Kiungu. Lakini kwa kweli kuna. . .

19 [Ndugu fulani anaongea na Ndugu Branham kuhusu mfumo wa sauti—Mh.] (Vema, bwana. Asante.)

20 Kwa kweli, hakuna kitu kama m—mponyaji wa Kiungu, kwa kuwa Kristo ndiye huyo Mponya. Unaona? Na hakuna kitu kama mwokozi wa Kiungu, miongoni mwa wanadamu. Kristo ndiye huyo Mwokozi. Basi wazia tu, kwamba kila mtu ambaye amepata kuokoka, ama atawahi kuokoka, aliokolewa Kalvari. Hapo ndipo ambapo, "Alijeruhiwa kwa makosa yetu, na kwa mapigo Yake tuliponywa." Papo hapo, tuliponywa.

21 Sasa, kitu cha pekee ni, kuhubiri Neno. Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, aliwaagiza wanafunzi Wake kuenda ulimwenguni

kote na kuhubiri Injili kutoka hapo, akisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio."

22 Na daima tunakuta matabaka matatu ya watu miongoni mwa kusanyiko, hayo ni: waaminio halisi, wanaojifanya waaminio, na wasioamini. Kwa hiyo sisi... Wote wamechanganyikana hapo. Walikuwa nao katika siku Yake. Tunao sasa.

23 Lakini mwaminio halisi hajaribu kutafuta hotuba fulani mashuhuri ya kielimu, au mtu fulani aliyevalia vizuri, ama mwalimu fulani na nafsi yake jukwaani. Lakini kwa imani rahisi... Kristo ni rahisi sana, hata, wenye hekima wanapita juu yake. Hawaipati kamwe. Na, hata hivyo, ni rahisi kama—kama mkono wako wa kulia. Unajua, Yesu alimshukuru Baba kwa ajili ya hilo wakati mmoja, kwamba, "Alikuwa amewaficha mambo haya wenye hekima na akili, na kuwafunulia watoto wachanga ambao watajifunza." Unaona?

24 Basi leo hii, wakati makanisa yetu yanapokuwa maonyesho mengi ya Hollywood, badala ya Injili wazi tu ya kawaida, unaona, imekuwa ni maonyesho ya mavazi, na ninii—na mtindo wa kiakili, mpaka inaonekana kuwatatanisha watu. Bali ni—ninaipenda tu jinsi Biblia ilivyo nayo hapa, urahisi tu, kuamini kazi ilimalizwa na Yule mkuu, Yesu Kristo, na Yeye tunampenda na kumpa sifa.

25 Sasa hebu tuzungumze juu Yake, ila kwanza hebu tusome baadhi ya Neno Lake. Ninapenda kusoma Neno Lake, kwa kuwa Biblia ilisema, kwamba, "Imani huja kwa kusikia, kusikia Neno la Mungu." Sasa, sisi, ni wangapi wanaamini Neno la Mungu? Hebu tuone. Loo, hilo ni jema. Kama tunaliamini Neno hilo, hiyo ndiyo yote itupasayo kufanya, kama tunaamini Hilo. Sasa, hilo ndilo jambo kuu, kama tunaamini Hilo.

26 Basi sasa tazama, kama siku zinavyoenda, inanibidi kubadilisha. Inanibidi kusema, "Vema, mwaka jana ni—ni—nilifanya jambo fulani, bali sikulifanya vizuri. Nimejifunza zaidi juu yake." Unajifunza. Sote tunajifunza; sayansi inafanya hivyo. Sayansi itatoa kitu fulani, waseme, "*Hili* liko hivyo kisayansi." Na katika mwaka mmoja, kisayansi haliko hivyo. Lakini shida yake ni kwamba, na wao, hawatakubali hilo. Lazima tulikubali, na kusema kwamba tumekosea. Unaona?

27 Lakini, lipo jambo moja kuhusu Mungu, Yeye hafanyi makosa. Basi uamuzi Wake wa kwanza ndio uamuzi Wake pekee, kwa sababu Yeye hana kikomo. Na ili kuwa asiye na kikomo, hiyo ni kamilifu mara kamilifu, ongezea kamilifu. Na, kamilifu, ni bila kikomo. Yeye alijua mambo yote tangu mwanzo. Haimbidi kughairi hata neno moja. Haimbidi kuboreka, kwa sababu uamuzi Wake wa kwanza ndio uamuzi pekee unaoweza kufanywa. Yeye hajifunzi zaidi, kuwa mwerevu zaidi,

tunavyodai tunakuwa. Lakini Yeye alikuwa mkamilifu, kwa kuanzia.

28 Kwa hiyo, basi, wakati chochote tunachosoma katika Biblia, ambacho, tunaamini kwa dhati kuwa ni Neno la Mungu. Na wakati tunaposoma Hilo, tunaweza kutuliza nafsi yetu moja kwa moja juu ya Hilo. Mungu kamwe hawezi kubadilisha Hilo. Yeye akibadilika, basi Yeye ni—Yeye yuko tu kama nilivyo mimi, unaona, Yeye ana kikomo, na Yeye amejaa makosa. Lakini Yeye hana kikomo. Yeye ni asiye na kikomo, na Yeye hawezi kukosea.

29 Hivyo basi, wakati mtu wa kwanza akimjia, pamoja na shida uliyo nayo usiku wa leo, kama ni kwa ajili ya wokovu, mpango ambao Mungu aliweka, kumwokolea mtu huyo, ndio mpango ule ule ambao Yeye hukuokoa nao. Na Yeye alikuwa na mpango mmoja, na huo ulikuwa ni kupitia damu iliyomwagika. Na mtu alikuja Kwake kwa ajili ya ugonjwa, juu ya msingi Yeye aliomponya mtu huyo, Yeye daima inambidi kudumisha kitu hicho hicho. Kama alitenda juu ya jambo fulani, njia moja wakati mmoja, na njia nyingine wakati mwingine, basi usingejua jinsi ya kumwendea Yeye. Bali, unaona, Yeye hana budi kutenda vile vile hasa kila wakati, kwa hiyo sisi tuna imani na Yeye. Unaona?

30 Basi ikiwa kitu chochote hakifanyiki, ambacho tumeomba, lazima tuchunguze tena na kuona mahali ambapo mkondo umekwamia. Unaona? Kuna kitu kilicho kasoro, mahali fulani. Labda presha nyingi kupita kiasi imeunguza fyuzi, unaona. Bali sisi—sisi inatubidi kunyosha kitu hicho. Na halafu kama kila . . . kama ninii yetu . . . Kama roho zetu hazituhukumu. Unaona? Kama hatuhukumiki, basi tuna kibali kwa Mungu, tunajua tunaenda kupata kile tunachoomba. Tuna haja yetu kwa sababu hatuhukumiki.

31 Lakini tunapohukumiwa na kutokuamini, dhambi ya aina yoyote . . . Na dhambi ni kutokuamini. Kuna aina mbili pekee, vitu viwili ambavyo kila mtu ulimwenguni anaishi kwavyo, hivyo ni, ama imani au kutokuamini. Hakuna njia nusu katikati. Hakuna mtu mlevi asiye mlevi usiku wa leo. Hakuna ndege weusi weupe usiku wa leo. Na hakuna wenye dhambi watakatifu. Ni ama umezaliwa mara ya pili au hujazaliwa mara ya pili. Sisi ama tunaamini au hatuamini.

32 Hivyo basi, ninaamini, kwamba, wakati Yesu anapoihukumu dunia . . . Ambayo, Mungu ataihukumu dunia kwa Yesu Kristo. Ninaamini kwamba tutahukumiwa na Biblia hii. Sasa, Mungu hawezi kuwa wa haki, kama tunavyoamini, na mkuu kama Yeye alivyo, na asiwe na kigezo fulani tunachohukumiwa kwacho.

33 Vema, kama wakisema tutaninii . . . "Yeye anaenda kuhukumu ulimwengu kwa kanisa." Sasa, ni kanisa lipi? Unaona? Katoliki wanasema, "Sisi ndio." Vema, Katoliki ipi? Vema, ya Rumi inasema, "Sisi ndio." Wayunani wanasema, "La,

la. Sisi ndio." Unaona? Na Methodisti wanasema, "Sisi ndio." Baptisti wanasema, "Sisi ndio." Na Pentekoste wanasema, "Sisi ndio." Na mwingine anasema, "Sisi ndio." Unaona? Lakini mimi . . . Hilo lingekuwa lenye kutatanisha kabisa. Watu wasingejua kitu cha kuamini.

34 Bali, "Hapo mwanzo alikuwa Neno, naye Neno alikuwa pamoja na Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Nalo Neno lilifanyika mwili likakaa katikati yetu," yeye yule jana, leo, na hata milele. *Hii* ndiyo hukumu yetu inatoka kwayo, Biblia, kwa hiyo hebu kwa uchaji tuamini kila Neno.

35 Nami nimesema, tukio hilo halisi, la kuzaliwa upya litaitikia kila ahadi ya Mungu kwa "amina." Hawatajaribu kusema, "Vema, hilo lilikuwa kwa ajili ya siku nyingine," au, "Hilo si kwa ajili yetu. Roho Mtakatifu alikuwa kwa ajili ya watu huko nyuma katika siku nyingine." La, la.

36 Petro alisema, kwenye Siku ya Pentekoste, "Ahadi ni kwa ajili yenu, kwa watoto wenu, kwa wale walio mbali, hata wote ambao Bwana Mungu wetu atawaita."

37 Yesu aliliagiza kanisa Lake, kasema, "Nendeni ulimwenguni kote na kuhubiri Injili. Yeye aaminiye na kubatizwa ataokolewa. Yeye asiyeamini atahukumiwa, na," ni kiunganishi, "ishara hizi zitafuatana na hao waaminio: katika Jina Langu watatoa pepo; watanena kwa lugha mpya; watachukua nyoka, au kunywa vitu vya kufisha, havitawadhuru; wataweka mikono yao juu ya wagonjwa, nao watapata afya." Sasa, hilo—hilo ama ni sahihi au si sahihi. Kwangu mimi, mimi ni rahisi. Ni—ninaamini tu ni sahihi, na hayo ndiyo yote inipasayo kuambatana nayo. Wale ambao hujaribu kuelezea hilo mbali, si—siwezi kuona hilo. Ninaamini kwamba ni Neno la Mungu, na hilo ni Kweli.

38 Sasa, huenda nisiwe na imani ya kutosha kufanya hayo yote yafanye kazi, bali kwa hakika nisingetaka kumzuia mtu yeyote ambaye alikuwa na imani tosha. Huenda nisiwe na imani ya kutosha kuwa kama Henoko, ambaye alifanya matembezi ya alasiri pamoja na Mungu, na haikumlazimu kufa, alitembea tu akaenda Nyumbani. Bali kwa hakika ningependa kuona mtu fulani akilifanya sasa, mwajua. Kwa—kwa hakika nisingetaka kumzuia, kufanya hivyo. Ninaomba kwa ajili ya imani ya aina hiyo, maana hiyo ndiyo aina ya imani ambayo inaenda kutubidi kuwa nayo. "Sisi tulio hai na tumesalia kwenye Kuja kwa Bwana tutabadilishwa katika dakika moja, katika kufumba na kufumbua jicho, na kutwaliwa juu pamoja na wafu waliofufuka, kumlaki Bwana hewani, na daima tutakuwa pamoja na Yeye." Hiyo ndiyo shauku ya moyo wetu.

39 Sasa, hebu tugeuke sasa kwenye Mathayo, mlango wa 8, na kuanzia na kifungu cha 23, kusoma se—sehemu ndogo ya Maandiko hapa, kwa ajili ya kupata muktadha, ama fungu, hasa, kwa ajili ya muktadha wa Ma—Maandiko machache

niliyoandika hapa chini, ambayo ninataka kurejea, na matamshi fulani, muhtasari. Mathayo 8:23, kuanzia, na kusoma kifungu cha 27, vyote pamoja.

*Akapanda chomboni, wanafunzi wake wakamfuata.*

40 Ninapenda hilo. Walimfuata Yeye popote Yeye alipoenda.

*Na, tazama, kukawa na msukosuko mkuu baharini, hata chombo kikafunikizwa na mawimbi; naye alikuwa amelala usingizi.*

*Wanafunzi wake wakamwendea,* wakamwamsha, *wakisema, Bwana, tuokoe, tunaangamia.*

*Akawaambia, mbona mmekuwa waoga, Enyi wa imani haba? Mara akainuka, akazikemea pepo na bahari; kukawa shwari kuu.*

*Wale watu wakamaka wakisema, Huyu ni mtu wa namna gani hata pepo na bahari zamtii!*

41 Sasa, Bwana akipenda, ninataka kuchukua kifungu kidogo tu kifupi kutoka hapo; linasikika kwa namna fulani la kigeni, maneno matatu: *Nenda, Kamwamshe Yesu,* au, "Kumwita Yesu jukwaani."

42 Sasa, hii ilikuwa ni kwenye wakati wa ajabu wa mkutano wa Bwana wetu, au huduma Yake ya duniani. Na mimi ninaamini kwamba huduma Yake ya duniani haijakoma, kwa sababu Yeye yuko ndani ya watu Wake sasa. Mungu alikuwa ndani ya Kristo; Kristo ndani ya watu. Na Yeye anafanya kazi Zake zile zile sasa ambazo Yeye alifanya wakati ule. Kwa hiyo Yeye alijaribu, na alikuwa mchovu wa siku, katika mlango uliotangulia, kulingana na—na Marko 4:35. Tunakuta hapo kwamba Yeye alikuwa amemponya mama ya mke wa Petro kutokana na homa, na kulikuwa na miujiza mingi mashuhuri ambayo Yeye alikuwa amefanya.

43 Na sisi tunapata hapa kwamba Yeye alikuwa anafundisha katika methali, siku zote akienenda katika kufanya maagizo ya Baba. Na ingekuwa vyema kama sisi sote tulimchukua Yeye kwa ajili ya mfano wetu: siku zote kwenye shughuli za Baba.

44 Na hapana shaka lazima Yeye alikuwa amechoka na ni mchovu, katika safari Yake. Na mimi ninamwona Yeye, Yeye alikuwa na haja kuvuka Galilaya. Na wakati Yeye anapoanza kuvuka, amechoka na ni mchovu, nguvu zilikuwa zimemtoka, kutokana na mambo haya yote ambayo Yeye alikuwa amefanya, kuhubiri, kuwaombea wagonjwa.

45 Na Yeye alijua, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mungu, na Yeye alijua kulikuwa na kazi kubwa mbele. Alijua kulikuwa na mwendawazimu huko Gadara, ambaye alishakuwa mtu wa mwituni kwa miaka, jamaa mdogo, kama tunavyoambiwa, ambaye alikuwa amepoteza fi—fikira zake za kibinadamu, na kuishi huko nje makaburini akiwa na roho mwovu. Na ni

mahali pa jinsi gani kwa mwanadamu kuishi, makaburini, lakini panafaa sana kwa ibilisi kuwa kati ya vitu vilivyokufa. Kwa hiyo aliishi huko nje, na alikuwa ameteswa vibaya sana na pepo hawa, mpaka wao—wao (yeye—yeye) alikata minyororo, na nguvu zake zilikuwa nguvu kuu.

46 Na hivi mliwahi kumwona mtu ambaye alikuwa amepagawa roho mwovu namna hiyo? Yeye ana nguvu mara nyingi kuliko nguvu zake. Jinsi ambavyo nimewaona katika mikutano, wakati makundi ya polisi hata wasingeweza kuwashika. Wangewararua hao polisi vipandevipande, na kuwatupa kando, na—na kutoka nje kuingia kwenye . . . na kufanya yasiyofaa.

47 Yeye kwa mbali . . . Kwa sababu amejisalimisha kabisa kwa huyo mwovu, alimmiliki, na yeye hakuwa na ufahamu wake mwenyewe. Alifanya tu kile roho huyo mwovu alichoweka ndani yake kufanya.

48 Ndipo nikawaza, kwa kujisalimisha kikamilifu kwa ibilisi, kunaweza kumpatia mtu labda mara tano ya nguvu zake, kujisalimisha kikamilifu kwa Mungu kungemfanyia nini mtu? Kungemfanyia nini kiwete ambaye ni dhaifu katika mwili, na hawezi kutembea, au kitu fulani? Kama tungejisalimisha kikamilifu kwa Roho Mtakatifu, atupe nguvu kuu, kuinuka katika Jina, maana, "Aliye ndani yenu ni mkuu kuliko yeye aliye katika ulimwengu." Mnaona? Nyinyi . . . Ngu—nguvu katika Mungu, zilizoko ndani yenu, ni kuu kuliko mateso yoyote yawezayo kuja juu yenu. Hakuna kitu kiwezacho kukushinda, kiwezacho kukuzidi, kwa sababu umejawa nguvu kuu. Na hizo nguvu kuu ni Roho Mtakatifu ambaye hutamalaki maisha yako, ikiwa wewe ni Mkristo.

49 Na kazi hii kubwa ilikaa kati Yake na siku iliyofuata, na Yeye alijua hili. Basi kwa hiyo wakati chombo kikivuka bahari, Yeye alichukua fursa hiyo kwa ajili ya pumziko dogo. Sasa, ndugu, mchungaji hapa, na wahudumu wengine, wanajua kile inachomaanisha kati ya mkutano wa asubuhi na mkutano wa alasiri. Mara nyingi, hasa unapopata maili chache ngumu kama nilizo nazo, ungependa kulala chini na upumzike dakika chache, mwajua, umechoka tu.

50 Pia kumbukeni, Yesu alikuwa mwanadamu; mwanadamu sana, hata Yeye aliweza kufa; mwanadamu sana, Yeye aliweza kulia; mwanadamu sana, Yeye aliweza kuona njaa. Alikuwa, kwa hali moja, mwanadamu, kwa sababu Yeye alikuwa ni Mwana wa Mungu aliye muumba. Mungu alikaa ndani Yake. Sasa, lakini Yeye alikuwa mwanadamu. Na Yeye alikuwa ni mwanadamu na Mungu, pamoja. Mungu aliumba Seli ya damu katika tumbo la uzazi la bikira Mariamu.

51 Ambayo, tunajua damu inatoka, himoglobini, hutokana na jinsia ya kiume. Kuku anaweza kutaga yai, ndege; lakini ikiwa

hajakuwa na wa kiume, halitaanguliwa. Si rutubifu. Kwa hiyo hutokana na wa kiume.

52 Basi katika kisa hiki, wa kiume alikuwa ni Mungu, Roho, Yehova, Baba. Na Yeye alimtia uvuli bikira na kuumba Seli hii ya damu ambayo ilimzaa Mtu, Kristo Yesu, ambaye alikuwa ni Mwana wa Mungu. Sasa, Yeye alikuwa si Myahudi wala Mtaifa. Alikuwa Mungu. Maana, unaona, Yeye hakuwa damu ya Kiyahudi, wala Yeye hakuwa damu ya Mataifa. Alikuwa Damu ya Mungu, Damu umbaji kutukomboa sisi. Kwa hiyo hakuna Myahudi wala Mtaifa awezaye kusema Yeye alikuwa wetu ama lile. Yeye alikuwa wa . . . Alikufa kwa ajili ya jamii iliyoanguka ya Adamu, kwa ajili ya pande zote mbili, kwa ajili ya watu wote, kila mahali, ambao wangemwamini Yeye.

53 Sasa, akichukua pumziko hili fupi, wanafunzi Wake walirudi kwenye makasia yao. Na mimi ningewazia walikuwa wanamaji kwelikweli kwa sababu walizaliwa hapo baharini, na kukuzwa hapo, na walijua ma—mambo yote ya baharini na maji haya hatari, na mahali mawimbi yalipokuwa, na mahali samaki walipokuwa, na saa na nyakati. Kwa hiyo walichukua makasia yao na kumfuata Yeye. Alikuwa anaenda huko Gadara. Alikuwa tu amemaliza uamsho upande huu mwingine, kwa vile alikuwa anaenda kuvuka bahari.

54 Sasa, akiwa amechoka, Yeye anaenda huko nyuma ya chombo, na—na mmoja wa waandishi alisema Yeye alilala chini kwenye mto: hapana shaka alikuwa amechoka. Basi wewe wazia tu kwa dakika chache, na jinsi Yeye alivyofanya kazi ili kutuokoa sisi. Mambo haya yote yalikuwa kwa ajili ya manufaa yetu. Ndipo Yeye anaenda nyuma, kujilaza chini. Sasa, wanafunzi . . .

55 Uamsho umekwisha. Uamsho wa siku hiyo umemalizika, na sasa wamerudi kwenye kazi yao ya kupiga makasia na kuendesha chombo. Na hapana shaka walikuwa wakishangilia juu ya kazi ambazo walikuwa wamemwona Yeye akifanya. Kazi ambazo Yeye alikuwa amefanya, hapana shaka walikuwa wakijadili matendo Yake, kwa sababu Yeye alikuwa huko nyuma katika chombo, amelala.

56 Na mimi ninafikiri kwamba, yote hayo, yanalingana na wakati huu ambapo tunaishi, unaona, uamsho ambao ndio kwanza tumalize, uamsho huu wa kipentekoste, uamsho mkuu wa uponyaji ambao ulitikisa ulimwengu mzima kote. Hebu wazia tu, mioto ya uamsho inawaka juu ya kila kilima kote ulimwenguni, kote na kote ulimwenguni. Mimi huusafiri, kila mara. Ninajiandaa kufanya ziara nyingine ya ulimwenguni. Na katika kila nchi, na katika kila taifa, mioto ya uamsho wa kipentekoste inawaka. Wapresbiteri wanaipokea, Wabaptisti, Walutheri, Wamethodisti. Kwa hakika ni zamu ya mwisho ambapo Mungu anawaita watu Wake. Na mioto hii mikubwa ya uamsho inawaka.

57 Na hawa wanafunzi, kama tulivyo leo hii, uamsho ulikuwa umeisha. Na wao walikuwa wamekusanyika mbele ya chombo, labda, ama kwenye makasia yao, na walikuwa wanazungumza kuhusu kile Yeye alikuwa amefanya, kazi Zake, ambazo zilimtangaza Yeye wazi kwao, kuwa kile Yeye alichodai kuwa.

58 Sasa, mnajua, mtu anaweza kudai kuwa karibu kitu chochote. Lakini hiyo siyo ishara kwamba wao ni kile wanachodai kuwa. Unaona? Tu—tunaona hilo katika kila mkondo wa maisha. Tunakuta wauzaji wanaodai kuwa wauzaji, na wao sio. Tunakuta fundi wa umeme wanaodai kuwa fundi wa umeme, na wao sio. Tunakuta makanika ambao wanadai kuwa makanika, na sio. Na tunawakuta watu ambao wanadai kuwa Wakristo, na sio.

59 Yesu alitaja wazi kile Mkristo alichokuwa. Unaona? "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio," unaona, kile ambacho watafanya, kile ambacho Kanisa linaloamini litafanya. Na Yeye akiwa ni Mungu, na asiye na kikomo, Yeye—Yeye—Yeye alisema, "Mbingu na nchi zitapita, bali Neno Langu halitashindwa kamwe." Kwa hiyo, lazima libaki hivyo daima. Yeye alilisema. Ninaliamini.

60 Sasa, wanafunzi wakijadiliana wao kwa wao, kile kazi Zake, zilikuwa zimefanywa, na jinsi ambavyo watu walikuwa wamezipokea. Hayo huenda yalikuwa ndiyo mazungumzo yao, kuhusu Yeye kuwa Masihi. Na hakukuwa na shaka katika nia za watu wengine. Kwa mfano, huenda walisema, "Sasa, Musa alisema Bwana Mungu wetu atamwinua nabii kama yeye. Yeyote yule ambaye hatamsikiliza nabii huyu akatatiliwa mbali kutoka kwa watu. Sasa, tunajua kwamba Masihi alikuwa anaenda kuwa Mungu-Nabii. Alikuwa anaenda kuwa Mtu ambaye angekuwa Na—Nabii mkuu. Angekuwa ndiye Mungu wa manabii, bali, hata hivyo, katika matendo, Yeye angekuwa Nabii, kwa sababu Neno la Mungu huja pekee kwa nabii. 'Neno la Mungu humjia nabii.'" Sasa, na halafu Yeye akiwa. . . Hilo lilikuwa tu ni Neno ambalo liliwajia manabii, bali Yeye alikuwa ni Neno. Unaona? Hiyo ndiyo tofauti. Kwa hiyo ilibidi Yeye awe ni Nabii.

61 Na hapana shaka kwamba walikuwa wamejadiliana kuhusu wakati, Simoni, wakati alipomwona Yeye kwa mara ya kwanza, na Yeye akamwambia kuwa yeye alikuwa ni nani, nini lililokuwa jina la baba yake. Basi, mbona, alijua kwamba Mtu huyo hakumjua, kwa hiyo alijua huyo lazima awe ni nabii. Na halafu wakati Filipo alipoona hili, na kuenda na kumwambia Nathanaeli, naye Nathanaeli akarudi kuona, na kile kilichokuwa kinaendelea. Basi Yesu alizungumza naye na kusema, "Tazama Mwisraeli," huko nje kwenye kusanyiko, mwajua, akiwa amesimama na Filipo, kasema, "ambaye hamna hila ndani yake."

62 Akasema, “Rabi, ulinijua lini Wewe?” Maneno mengine, hiyo ilikuwa mara ya kwanza waliwahi kumwona Yeye.

63 Yeye akasema, “Kabla Filipo hajakuita wewe, wakati ulipokuwa chini ya mti, nalikuona.” Loo, jamani!

64 Akasema, “Rabi, wewe ni Mwana wa Mungu. Wewe ni Mwana wa Mungu, Mfalme wa Israeli.” Sasa, hilo lilimfanya Yeye Masihi.

65 Ndipo basi, bila shaka, kulikuwa na baadhi ya waothodoksi mashuhuri wamesimama karibu, ambao hawakuamini hili. Na iliwabidi kujibu kusanyiko lao. Walisema, “Mtu huyu ni Beelzebuli. Yeye ana roho ya Beelzebuli.” Na Beelzebuli alikuwa ni ibilisi, ambaye ni mpiga ramli, ama mchawi. “Na hivyo ndivyo yeye hufanya hilo. Ni kuwasiliana kimawazo, kwamba anasoma akili zao kupitia uchawi ama kitu fulani katika utaratibu huo, na hili humfanya ibilisi.”

66 Yesu alikuwa amewaambia kwamba namna zote za kukufuru zitasamehewa mwanadamu, isipokuwa kukufuru Roho Mtakatifu. Mnaona? Na Roho Mtakatifu hakuwa ametolewa bado. Kwa hiyo wakati Roho Mtakatifu angekuja, na angekuja baada ya Upatanisho kufanywa, na kufanya kazi ile aliyofanya Yesu, ingekuwa ni dhambi isiyosameheka kumwita huyo roho mwovu. Wazia hilo. Unaona? Baada . . .

67 Yesu, Yeye alikuwa hapo kudhihirisha Neno. Mwanadamu alikuwa angali katika dhambi, akiwa tu na sadaka ya mnyama. Na uhai wa mnyama haungeweza kuja juu ya mwaminio, kwa sababu alikuwa ni mnyama, na huyu alikuwa mwa—mwanadamu. Naye mnyama hana nafsi; mwanadamu anayo. Na huyu hapa alikuwa Mfalme wa nafsi, Mungu Mwenyewe, akidhihirishwa katika utu wa Mwana Wake, Yesu Kristo. Na wakati Yeye alipokufa, Roho wa Mungu alirudi juu ya mwaminio. Ndipo basi mtu aliye na nafasi ya kupokea Hili, na halafu aite kazi ya huyo Roho, “ibilisi,” haisameheki. Kamwe haiwezi kusameheka.

68 Sasa, maskini mama yangu aliye wa kusini, wakati nilipokuwa mvulana mdogo, kabla sijaongoka, alikuwa ni mwanamke mzuri wakati huo.

69 Nilikuwa na majaliwa ya kumwongoza mama yangu kwa Kristo, na kumbatiza, na kumwona akifa, nilishika mikono yake wakati alipokufa, na kuzungumza kuhusu Yesu hadi hata asingeweza kuongea tena, kusifu Jina Lake. Nikasema, “Mama, kama ungali unampenda Yeye, konyeza macho yako,” na yeye akayakonyeza tu macho yake, na machozi yakitiririka chini mashavuni mwake, wakati alipoenda kukutana na Mungu.

70 Na yeye alizoea kuniambia, kabla ya yeye kujua bora zaidi, “Billy, wakati ku—kumkufuru Roho Mtakatifu ndiko dhambi isiyosameheka,” akasema, “hiyo inamaanisha mwanadamu ambaye angeuondoa uhai wake mwenyewe, hawezi kusamehewa

hilo." Hilo lilikuwa ni wazo lake kulihusu. Bali baadaye tunaelewa kwamba *kufuru* ni "kucheka, au kudhihaki, kuzungumza juu ya na kudhihaki Roho Mtakatifu."

71 Ndipo Yesu hapa aliwaambia, kasema, "Mnaweza kusema mambo hayo na kuniita Beelzebuli, hilo, nitawasamehe hilo. Bali ajapo Roho Mtakatifu baada ya mimi kuondoka, basi haisameheki, ku—kumkufuru huyo. Na wakati Yeye anapokuja. . ." Yeye, ambaye si wazo, sasa, ni Mtu. *Yeye* ni kiwakilishi nafsi. *Yeye* ni Mtu. "Basi wakati Yeye ajapo, Yeye hatasamehe makosa yenu kwa sababu ya hilo. Mnaona? Yeye kwa kweli atazifanya kazi nizifanyazo. Ataendeleza huduma Yangu. Na Yeye atawafundisha mambo haya ambayo nimewafunza, na atawaonyesha mambo yajayo." Mnaona?

72 "Kwa kuwa Neno la Mungu," Waebrania 4, "ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, hukata na kugawanya hata kwenye mafuta ya mfupa, na Mtambuzi wa mawazo yaliyoko moyoni." Roho Mtakatifu hutambua, unaona, kwa sababu Yeye ni Neno. Yeye ni Neno. "Nalo Neno la Mungu ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Mtambuzi wa mawazo na makusudi ya moyo." Loo, walipaswa kuwa wamejua hilo.

73 Kisha, kisha mambo haya yote waliyojadili, na jinsi yule mwanamke kisimani alivyotokea, na mambo mengine mengi, Bartimayo kipofu, na mambo ambayo walikuwa wamemwona Yeye akifanya. Ndipo basi hapana shaka walikuwa wanajadili hayo. Na wao walishawishika kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi, hakuna mtu mwingine angaliweza kuchukua mahali Pake.

74 Kwa sababu gani? Walikuwa hawajakuwa na nabii duniani kwa mamia na mamia ya miaka. Ndipo mara ghafla, akainuka nabii jina lake Yohana, asiyechukua sifa mwenyewe, bali akitamka hili, akitangaza hili, hasa, kwamba, "Masihi yuko moja kwa moja miongoni mwenu sasa. Mnaona? Yupo Mtu aliyesimama miongoni mwenu." Loo, jamani! Alikusudia kwamba wao wangejua kwamba wakati ulikuwa umewadia.

75 Yohana Mbatizaji alikuwa ni mtu mashuhuri. Mnajua kuzaliwa kwake, na jinsi alivyopokea Roho Mtakatifu kabla hajazaliwa, ndani ya tumbo la mama yake.

76 Wakati, Mariamu alipokuja, akiwa ni bikira, na kumwambia kwamba alikuwa anaenda kumpata mtoto, na kumwambia Elisabeti kuhusu kupata mtoto, na kuhusu jinsi ambavyo Roho Mtakatifu alikuwa amemtokea, Malaika wa Bwana, hasa, na alikuwa amemwambia kwamba yeye alikuwa mja mzito pia. Ndipo yeye akasema, "Ninaenda kumpata Mtoto mwanaume, na nitamwita Jina Lake Yesu." Na wakati yeye aliposema, "Yesu," mara ya kwanza ambapo hilo Jina liliwahi kutajwa katika midomo ya binadamu. Mtoto mdogo ndani ya tumbo la mama yake, amekufa, mama alikuwa na wasiwasi juu yake. Hakuna

uhai, miezi sita, hilo kwa jumla si la kawaida. Bali punde tu Jina hilo "Yesu" lilipotamkwa kwa mara ya kwanza kwa mdomo wa mwanadamu, maskini huyo Yohana, aliyekufa katika tumbo la mama alifufuka na kuruka kwa furaha, Biblia inasema.

77 Kama litafanya hilo kwa mtoto aliyekufa, linapaswa kufanya nini kwa Kanisa lililozaliwa mara ya pili ambalo limejaa na Roho Mtakatifu? Kuponya wagonjwa, kuokoa waliopotea! Unaona? "Kwa kuwa punde tu salamu hizo zilipoingia masikioni mwangu, mtoto wangu aliruka kwa furaha tumboni," mnaona. Na yeye alikuwa amejaa Roho Mtakatifu kutoka tumboni mwa mama yake. Na mtu huyu aliyejazwa Roho Mtakatifu. . .

78 Ingawa, baba yake alikuwa kuhani. Kwa kawaida, ilikuwa ni desturi katika siku hizo kwa mtoto kufuata desturi ya baba yao, ama kazi ya baba. Na sasa tunakuta kwamba Yohana, kazi yake, ilikuwa muhimu sana asingeweza kuenda kwenye shule ya makuhani ambayo baba yake alihudhuria, kwa sababu wangekuwa wanasema, "Sasa, mnajua, Ndugu *Nanii* hapa inabidi. . . Wewe unapaswa kumtangaza Masihi. *Huyu* Ndiye. Mbona, unajua *huyu* Ndiye, kwa sababu, tazama, yeye ni jamaa mwema sana."

79 Lingekuwa karibu sawa na chaguo ambalo wanafunzi walifanya juu ya ni nani angechukua mahali pa Yudasi. Unaona? Ilimwangukia Mathias. Walimchagua Mathias, kwa kura, bali Mungu alimchagua Paulo. Unaona? Ilikuwa tofauti.

80 Tazama. Pia tunakuta kwamba kazi yake ilikuwa muhimu sana, hata akaenda nyikani na kukaa huko mpaka alipokuwa na umri wa miaka thelathini. Ndipo wakati alipotoka nje, akihubiri, alijua aina ya Mtu ambaye huyu Yesu angekuwa. Kwani, a—alisimama hapo, na alikuwa na hakika kwamba Hiyo ilikuwa inaenda kuja katika siku yake, hata akasema, "Yupo Mtu aliyesimama miongoni mwenu, ambaye sistahili kubeba viatu Vyake. Yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na Moto."

81 Ndipo siku moja, akiwa amesimama pale, alitazama, na akaona ishara ikija kutoka mbinguni. Na alimjua Yeye, kwa ishara. Ndipo Yohana akashuhudia, akashuhudia hivi, "Ninashuhudia kwamba niliona Roho wa Mungu, kama hua akishuka kutoka mbinguni, na Sauti ikisema, 'Huyu ni Mwana Wangu mpendwa ambaye ninapendezwa ndani Yake.'" Alimtangaza Masihi kwa sababu aliona ishara ya Masihi.

82 Sasa, hawa wanafunzi hapana shaka walikuwa wakijadili hili, baada ya uamsho huu kuisha, mnaona, kwamba kwa ajili ya siku hiyo, mtazamo wa baadhi ya watu. Wengine wanaamini. Wengine hawaamini.

83 Hicho ndicho kitu kile kile tunachoona leo hii. Wapo watu ambao wanaamini. Wengine hawaamini. Tunalo katika—katika mikusanyiko yote: wengine waaminio; wengine hawaamini, hata kidogo.

84 Na wengine walisema, katika siku hiyo, "Hakuna mtu aliyewahi kunena kama Mtu huyu. Yeye hazungumzi kama kuhani au mhubiri. Kile Mtu huyo asemacho hutendeka pale pale. Unaona? Yeye hudhihirisha kile tunachohubiri juu yake. Unaona? Yeye, hakuna mtu aliyewahi kuzungumza namna hii." Vema.

85 Na kulikuwa na wasioamini fulani, kasema, "Mtu huyu ni Beelzebuli. Anaweza tu kufanya hili kupitia roho wa ibilisi." Naye Yesu alikuwa amewakemea.

86 Ndipo hapana shaka ilisema, Yohana, kijana, huenda ilisema, "Wazia hilo, ndugu, tunaye Huyo pamoja nasi sasa. Loo, ni wazo la jinsi gani! Yeye sasa yupo chomboni pamoja nasi."

87 Ikiwa sisi, usiku wa leo, ndugu yangu wa thamani na dada, tungeweza tu kutulia kwa dakika chache, kutambua, huyu Masihi ambaye tumenena habari zake, na Mungu alisema atakuja. Na alikuwa hapa duniani; akafa, akafufuka tena, akapaa juu Mbinguni. Na akarudi kwenye—kwenye—ninii... baada ya siku kumi, na kuonekana kwao kwenye Pentekoste, na kuagiza Kanisa Lake. Yesu yuyo huyo yu pamoja nasi leo hii tunaposafiri kwenye bahari adhimu ya maisha. Tunazungumza habari Zake. Tunawaza juu Yake. Tunasoma habari Zake, yale Yeye aliyofanya, kile Yeye alichokuwa, jinsi Yeye alivyoishi, aina za kazi Yeye alizofanya, na kisha tunasahau. Hivi mnatambua kwamba Yeye yu pamoja nasi, sio tu kuwa pamoja nasi, bali ndani yetu? Loo, jinsi ninavyowaza hilo!

Ni hisia jinsi gani ya usalama hapana shaka ilikuwa, kuwazia kuhusu Muumba Mwenyewe, akisafiri kwenye maji yaliyochafuka pamoja nao.

88 Loo, ni usalama jinsi gani ulio leo hii, kujua kwamba Mungu yeye yule aliyeumba mbingu na nchi, aliyeumba mavumbi haya tunayokaa ndani yake, yaitwayo miili, anasafiri chini katika bahari ya maisha pamoja nasi, tukijua kwamba ugonjwa na maumivu hutuhangaisha, na mauti hutuangalia usoni. Lakini tuna nini cha kuogopa? Muumba mwenyewe wa mavumbi yenyewe, elementi zenyewe kumi na sita zinazotufanya, petroli na nurulimwengu, anasafiri pamoja nasi kupitia kila dhoruba na kila bahari. Kweli yake kamwe haiwezi kushindwa. Yeye yu pamoja nasi, na alisema, "Tazama, niko pamoja nanyi daima, hata kufikia mwisho wa ulimwengu."

89 Sasa, wakisafiri kwenye maji haya yenye tufani, walikuwa wakijadili hili, na kuwazia kuhusu namna ya usalama ambao hapana shaka ulikuwa kwa watu waliokuwa pamoja nao, wanafunzi na kadhalika, kinachosumbua. Wanajua kulikuwa na uamsho mkubwa ulikuwa tu umefanyika, na wao walikuwa wanasherehekea juu ya matokeo yake.

90 Sasa, nafikiri hiyo inafanana kabisa kama sisi leo hii. Tumekuwa na uamsho mkubwa, bali, tunaona kwamba, unapoa.

Sasa, kulingana na historia, ambayo mimi si mtu mwenye elimu, ila nimechukua historia ya makanisa, *Baba Wa Nikea*, na *Babeli* kilichoandikwa na Hislop, na kadhalika, na kugundua kwamba uamsho wowote hukaa tu yapata miaka mitatu. Huo karibu ndio umbali ambao hukaa. Lakini huu umekuwa ukiendelea kwa karibu miaka kumi na mitano, kwa sababu nafikiri karibu ndio wa mwisho tutakaokuwa nao. Kwa hiyo tumekaribia Kuja kwa Bwana.

91 Basi kwa hiyo sasa labda uko jinsi walivyokuwa, kwenye kile chombo usiku ule, labda sisi ni kitu kile kile, kwamba sisi, wanafunzi Wake wanaomwamini Yeye, sasa tunasherehekea tu juu ya kile ambacho tumeona kikifanywa. Loo, mambo ambayo nimemwona Yeye akifanya! Ingechukua miezi na miezi, ku. . .Ningeweza kuandika vitabu vi—vingi, juu ya yale ambayo nimemwona Yeye akitenda, juu ya ishara kuu, maajabu, miujiza. Ambayo ni ninii tu. . .Imepita ufahamu wowote wa mwanadamu. Ilibidi iwe ni nguvu za kimbinguni za Mungu, kufanya jambo kama hilo.

92 Na si—sidhani kwamba ningeweza kusimama hapa juu ya dawati hili, kama mhudumu wa Injili, na ninge—na ningesema jambo ambalo si sahihi, nikiona kwamba nina umri wa miaka hamsini na minne na siku zangu zinaisha. Inanibidi kukutana na Yeye. Lazima niwe. . .Ninataka niwe mwaminifu kabisa. Mambo haya ni sahihi, na lazima yawe. Unaona? Kwa sababu, si hayo tu, bali ningekuwa ninawapotosha watu.

93 Bali nitasema, usiku wa leo, kwamba nilimwona Yeye. Amekuwa na ufanisi mwingi katika—katika jitihada zangu ndogo ndogo ambazo ninaweka. Sasa kumbukeni. Yeye amekuwa na ufanisi mwingi kuliko jitihada ambazo nimeweka kwa ajili Yake, kwa Injili Yake, kuliko Yeye alivyokuwa nao katika nchi Yake mwenyewe ambapo Yeye alitoka. Ni—ningeandika Biblia nyingi, kujua kile Yeye amefanya katika siku hizi za mwisho, kwa sababu Yeye aliahidi hilo.

94 "Mambo haya nifanyayo, nyinyi mtayafanya, na mengi kuliko haya mtafanya." Inasema "kubwa zaidi," ambalo, neno sahihi pale. Hakuna awezaye kufanya kubwa zaidi. Yeye alifanya kila kitu ambacho kiliweza kufanywa, unaona, kufufua wafu, kusimamisha maumbile, na kila kitu kingine. "Lakini mengi kuliko haya mtayafanya." Kwa kuwa Roho wakati huo alikaa ndani ya Mtu mmoja, Mwana wa Mungu, sasa wana wa Mungu wako kote ulimwenguni. "Mengi kuliko haya mtafanya, kwa kuwa ninaenda kwa Baba," unaona, kutuma Roho Mtakatifu kurudi juu ya Kanisa.

95 Na kwa hiyo lazima walikuwa wakati ule kama tulivyo sasa, kupumzika kati ya miamsho, wakingojea Kuja kwa Bwana. Na tunaposafiri tukiendelea, huku tukishuhudia, tukizungumza kuhusu, "Loo, ninakumbuka wakati tulipokuwa na mkutano

huu *huko*. Ninakumbuka wakati huu ulipokuwa *hapa*. Mtoto huyu aliyekufa akiwa amelala *pale*, na alikuwa amekufa siku mbili, na wao walimleta mkutanoni, na Roho Mtakatifu akamfufua moja kwa moja kuwa hai tena. Kumwona mtu huyu akiingia *hivi*, na *vile*, kipofu, amepindika, kiwete, akiteseka, kuwaambia yale waliyokuwa wametenda, na kile kilichokuwa kimetukia, jinsi Roho Mtakatifu alivyokutana na watu jukwaani, akawaambia yale waliyokuwa wamefanya. Wadanganyifu waliinuka na kufikiria ilikuwa ni kuwasiliana kimawazo, na kutajwa moja kwa moja. Na baadhi yao wakipooza, moja kwa moja mbele ya macho yetu, mbele za maelfu ya watu. Mambo haya yote makuu yakithibitisha hilo." Na sasa kwa namna fulani tunapumzika kati ya wakati, unaona, kupumzika.

96 Labda Yesu alikuwa anafanya wakati huo kama Yeye alivyofanya katika siku ya uumbaji. Aliumba nchi, na mbingu na nchi, katika siku sita. Na siku ya saba, Yeye alipumzika.

Unasema, "Je! huyo alikuwa Yesu?" Naam.

Biblia ilisema, "Yeye alikuwa ulimwenguni, na ulimwengu uliumbwa na Yeye, na ulimwengu haukumjua Yeye."

97 Kwa hiyo Yeye labda alikuwa anapumzika, kutoka uamsho mmoja hadi mwingine, kama tu Yeye alivyokuwa akipumzika kati ya Mwanzo na Kuja Kwake, unaona, akichukua pumziko fupi. Halafu, wakati Yeye alipokuwa anajaribu kupumzika, nao wanafunzi walikuwa . . . walikuwa wamesahau kuhusu Yeye kuwa pamoja nao, ndipo basi shida ikainuka.

98 Huo ndio wakati inapoanza. Wakati kanisa linaposahau kuhusu Uwepo wa Yesu Kristo, tunaposahau na kuanza kuzozana na kuhangaika, na kubishana kuhusu tofauti zetu za kimadhehebu, na kadhalika, huo ndio wakati hasa ambapo shida huanza.

99 Lakini mradi tu Kristo yupo, na Roho Mtakatifu anabariki watu wote, hatujali: rangi, kanuni ya imani, ama chochote kile. Sisi sote tuko katika kidimbwi kimoja kikubwa cha baraka za Mungu, tukishirikiana tu chini ya Damu ya Yesu Kristo, na hatutambui hilo.

100 Bali wakati tunapoanza kujaribu kuwazia, "Unajua, dhehebu langu ni bora kidogo kuliko lao, kubwa zaidi kidogo kuliko lao. Sisi tuna wafuasi wengi zaidi," hapo ndipo wakati shida inapoingia.

101 Kwa hiyo wanaanza kupata hiyo, na shida zikainuka wakati waliposahau kuhusu Yeye kuwa hapo. Kuzungumza sana kumhusu Yeye, na kukosa kutambua kuwa Yeye yuko pamoja nao. Laiti ningalikuwa na njia fulani ya kukazia hilo kabisa. Tazama, walikuwa wanazungumza kumhusu Yeye, bali walikuwa wamesahau kwamba Yeye alikuwa amelala ndani ya chombo hicho hicho walichokuwa ndani yake.

102 Pia leo hii, hilo ndilo ambalo limefanyikia makanisa. Tunazungumza kumhusu Yeye. Tuna mengi sana ya akili, mpaka watu wamefunzwa sana kwa Maandiko, mpaka wanaweza kuleta ujumbe ambao utaninii. . .Huwezi kuuwekea kidole. Lakini yuko wapi Mungu? Hilo ndilo ninalotaka kujua. Yako wapi hayo madhihirisho? Unaona? Mahubiri ya kiakili!

103 Biblia ilisema, "Kabla tu ya maangamizi ya gharika," na Yesu akasema, "ndivyo itakavyokuwa katika Kuja kwa Mwana wa Adamu, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu." Kulikuwa na majitu duniani. Walikuwa majitu, watu wakubwa kwa umbo.

104 Na leo hii kuna majitu wa kiakili. Wapo watu ambao ni, loo, watu mashuhuri, watu mashuhuri wenye uwezo. Wanajua Kiyunani kama tu wanavyojua Kiebrania, na kila kitu, na wanaweza kukiweka pamoja kwa werevu sana. Lakini uko wapi ule—ule uamsho? Yuko wapi Mungu yule ambaye huwasha moto kwenye moyo wa mwanadamu? Si jinsi ilivyo ya kiakili; inahitaji urahisi, kuleta nguvu za Mungu.

105 Ndipo wakapata, kama tulivyo nayo leo hii, kwamba shida iliingia. Chombo kikaanza kuyumbayumba, na upepo ukapeperushia mbali matanga, na maji yakajaza chombo. Kitu gani? Matumaini yote yalikwisha, matumaini yote ya kunusurika.

106 Sasa, kama uliwahi kamwe kuwa Galilaya, mambo yayo hayo hutendeka leo hii. Huko upande wa magharibi, kuna—kuna milima. Ufa ndani yake, namna *hiyo*, kwa njia fulani unakatwa na kuondolewa. Na, leo, wavuvi karibu na ufuo pale watakuambia kwamba ni hatari kuvuka bahari pale, kwa sababu hayo mawimbi huja bila kujua, na kufagia tu kabisa. Na hayo maji, maji yaliyotibuliwa, husukasuka tu kuzunguka na kuzunguka, na huzamisha wavuvi hata wa leo.

107 Ndipo mara ghafla jambo fulani likatokea. Shida ikainuka. Na matanga yakaanguka, na upepo ukayapeperushia mbali. Ndipo makasia yakaanza kushindwa, na kupasuka na kuvunjika, wakati hao wavuvi wenye migongo iliyo na nguvu waliyalalia, wakijua jinsi ya kukabili hayo mawimbi. Ndipo—ndipo ghafla chombo kikajaa maji. Lakini si ni ajabu kwamba watu, ambao saa chache tu zilizopita, amina, walimwona Yeye akifanya mambo kama hayo, na walikuwa wamesahau yote kuhusu hayo?

108 Mungu Yule aliyewafufua wafu, Mungu Yule aliyewaponya wagonjwa, Mungu Yule ajazaye na Roho Mtakatifu, ambalo tumeona likifanywa, sasa ni yule yule leo. Yupo papa hapa ndani ya chombo. Yeye yupo hapa pamoja nasi. "Tazama, niko pamoja nanyi siku zote. Kama ni katika shida, ama wakati kinaposafiri kwa shwari, ningali ndani ya chombo." Unaona?

109 Walikuwa wamesahau kuhusu hilo. Na walifikiri kupona kwote kulikuwa kumetoweka. Walifikiri wao. . .Walikuwa

wamemwona Yeye akifanya mambo mengi sana, lakini sasa walikuwa wamesahau Yeye alikuwa ndani ya chombo. Yote yalisahaulika, wakati wa shida, kama tu ilivyo sasa.

110 Sasa, kama tu leo hii, tunakuta, walipata matatizo ambayo weledi wao usingeweza kutatua. Unaona? Yalikuwa zaidi ya weledi wao kutatua. Wangejaribu kuinua juu matanga yao, na upepo ukayapeperushia mbali. Walijaribu kukaa kwenye makasia, kuzuia maji yasiingie kwenye mtumbwi, kupiga mawimbi sawasawa. Kama nyinyi mabaharia mnavyojua inawabidi kufanya, na si kuruka moja kwa moja juu ya wimbi, ungezamisha mtumbwi. Inakubidi kuuendesha, kusafiri kupitia wimbi unapopenya. Nao wavuvi, pamoja na yote waliyokuwa nayo, wakijali sana kunusurika, hata wakasahau kwamba Muumba alikuwa ndani ya chombo. Na weledi wao wote ungali ulishindwa.

111 Ninaona dada wawili wameketi hapa usiku wa leo katika viti vya magurudumu. Unaona, hapana shaka hao wanawake wamejaribu kila kitu ulimwenguni ili kupona. Huenda kuna watu hapa walio na kansa, mtu fulani aliye na ugonjwa wa moyo, na ujuzi wa daktari umefanya kila kitu wawezacho, kukusaidia. Lakini uko kwenye mwisho. Wao, hakuna kitu kiwezacho kufanywa. Hivi tumesahau ni Nani aliye pamoja nasi?

112 Ni nani huyu, anayesafiri bahari kuu la maisha, pamoja na sisi? Ni nani aliyetoa ahadi? Yeye ni Neno. Unaona? Halijawahi kuondolewa kwetu bado. Ninalitaka hivyo, moyoni mwangu, kama wakiwahi kuchukua *hiki*, ninalo Hilo *hapa*. Unaona? Unaona? Lakini Neno lingali pamoja nasi. Yeye ni Neno. Na ma—mambo ambayo daktari hawezi kutatua, mambo ambayo ulimwengu wa kanisa hauwezi kutatua, tunaye Muumba wa vitu vyote pamoja nasi.

113 Nilikuwa nikisoma barua ya tangazo iliyotolewa na Mpentekoste mashuhuri ambaye aliketi sako kwa bako na papa, si muda mrefu uliopita, katika baraza la ekumeni. Niliandika chini, miaka thelathini na mitatu iliyopita, kwamba jambo lilo hilo lingetendeka. Sasa, kamwe hutaweza kuwaingiza wapentekoste halisi, wa kiroho ndani ya kitu hicho. Wanajua bora kuliko hapo. Linasikika la kupendeza sana kwa wenye akili, bali nia ya kiroho inalishika upesi kwamba hilo ni kosa. Wanajua kwamba hilo ni kosa. Wanajua kile Mungu amesema kuhusu mambo hayo. Na kwa hiyo, wao, kamwe hawatalishika.

114 Sasa, wengine watalishika, ambapo Yesu alisema roho hizo mbili katika siku za mwisho karibu zingemdanganya Mteule mwenyewe kama yamkini. Unaona? Bali Wateule watajua tofauti. Ila tuko katika wakati wa shida ambapo hapana mhudumu ulimwenguni anayeweza kuzuia madhehebu yetu kujiunga na baraza hili la ekumeni. Tayari wako ndani yake. Haijalishi ni mambo mangapi ambayo Mungu alifanya, jinsi

Yeye alivyobarikiwa miongoni mwetu, waliingia moja kwa moja ndani yake, hata hivyo. Huwezi kulikomesha. Hayo tu ndiyo yote yaliyopo kulihusu. Wanaenda kufanya hivyo, sasa, matatizo yasiyoweza kutatuliwa na kanisa. Ndipo, punde tu tunapogundua kwamba . . .

115 Unaenda kwa daktari, yeye atasema, "Vema, ninasikitika kukuambia, lakini wewe—wewe una kansa." Vema, upesi, hayo ndiyo yote. "A—a—amekufa. Hayo tu ndiyo yote yaliyopo kuhusu hilo. Ama, yeye, wameenda." Madaktari wanasema, "Vema, huko ni kupooza. Huwezi . . . Hiyo ni lukemia." Vema, upesi sana, "Wao ni sawa na waliokufa, papo hapo." Unaona? Hofu inaingia, unaona, bali haipaswi kuingia.

116 Ni nani Huyu aliyetoa ahadi? Tunaishi kwa ajili ya nini? Ni kwa nini sisi ndio Kanisa la Mungu aliye hai? Ni kwa nini tumejazwa na Roho Mtakatifu? Kukumbuka katika wakati wa shida, Yeye angali hapa. Yeye hutuliza mambo. Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. Yeye yuko pamoja nasi vile vile tu. Huenda anapumzika dakika chache katikati ya mikutano, lakini Yeye angali hapa vile vile tu. Naam. Basi wakati shida inapoingia, na imani ya Yeye kuwa pamoja na sisi . . . Basi hofu inaingia. Na wakati hofu inapoingia, ndipo basi tunaingia katika shida kwelikweli.

117 Tunalo hilo katika kanisa, kitaifa, popote pale. Mataifa yote yanaogopa hata kufa. Yupo mwanaanga mahali fulani, na kuna bomu la atomiki. Na tunajua kwamba sayansi imetengeneza vitu vya kimitambo, mpaka kwamba, kwenye dakika yoyote, bila ilani, ulimwengu wote unaweza kuwa vipendevipende. Na ulimwengu unaogopa.

118 Mimi siogopi ulimwengu kuwa vipandevipande. Kunaenda kuwa na utawala wa Miaka elfu, baada ya huu kuisha. Mungu hatashindwa kusudi Lake mwenyewe. Kitu pekee ninachoomba, "Bwana, je! niko sahihi kwenda, wakati Yeye akija?" Hiyo ndiyo—hiyo ndiyo hofu pekee niliyo nayo. "Je! nimekupendeza Wewe, Bwana?" Unaona?

119 Usiogope kile mwanadamu anachofanya. Mwogope Mungu. Kasema, "Usimwogope yeye anayeweza kuangamiza mwili. Bali Yeye anaweza kuangamiza mwili na nafsi pia kuzimuni." Unaona? Hiyo ni kweli.

120 Sasa, mabishano na kadhalika, wakati shida inapoingia, woga. Na sisi tunaonekana kabisa kuwa vivyo hivyo leo hii. Bali, kumbukeni, Yeye angali pamoja na sisi.

121 Sasa, katika Yohana Mtakatifu, mlango wa kwanza, msisahau hilo, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, nalo Neno lilikuwa pamoja na Mungu, nalo Neno lilikuwa Mungu. Nalo Neno likafanyika mwili likakaa katikati yetu." Waebrania 13:8 ilisema, "Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele." Na Kitabu hiki ni ufunuo wa Yesu Kristo, kote kote kuanzia Mwanzo hadi

Kitabu cha mwisho, cha Ufunuo. Ni ufunuo wa Yesu Kristo. Manabii na mambo hayo yote yalikuwa yakimfananisha Kristo kimbele. Na kila kitu katika Kitabu ni Yesu Kristo.

122 Kwa hiyo, kumbukeni, Yeye angali pamoja nasi. Kila kitu, kurekebisha kila sababu ambayo ibilisi anaweza kuanzisha, ipo papa *hapa*. Tunayo, papa *hapa*. Shida; bali Bwana yuko ndani ya chombo. Vema. Wakiingia katika shida, ambapo madaktari hawawezi kurekebisha, kumbukeni, Yeye yupo hapa. Kama sisi. . . Msisahau. Yeye yuko ndani ya meli.

123 Walipaswa kuwa wanajua, wanafunzi hawa, kwamba Yeye alikuwa ndiye Masihi. Nalo neno *Masihi* linamaanisha "Yule aliyetiwa mafuta." Unaona? Basi ikiwa. . . Yeye alikuwa na Mungu wote ndani Yake. Mungu alikuwa ndani Yake. Akasema, "Mimi. . ." Yesu, Mwana, alisema, "Sifanyi lolote kwa nafsi Yangu ila lile nimwonalo Baba analitenda. Baba anaishi ndani Yangu." Unaona? Sasa ikiwa. . . Yeye alikuwa Masihi, kwa huo, pamoja na huo upako, ulimfanya Yeye Masihi kikamilifu. Na sisi, tukiwa na Roho yuyo huyo aliyekuwa juu Yake; si katika sehemu, bali ubora ule ule; pamoja na sehemu juu yetu, angetufanya sisi kama masihi wadogo, tungekuwa wana wadogo wa Mungu, wana wa Mungu waliopewa mamlaka. Na Roho Wake Mtakatifu ametutia muhuri ndani ya mwili Wake, na sisi ni watoto Wake.

124 Hakupaswi kuwa na kitu chochote kutusumbua, hakuna kitu cha kutuhangaisha. Sisi ni—sisi ni Wake. Kama sivyo, vema, sisi ni wasingiziaji wa uwongo, tu—tumekuwa tukishuhudia kitu ambacho hata sivyo. Ninaamini hilo. Ninaamini kwamba sasa sisi ni wana wa Mungu, si tutakuwa; sasa, sasa hivi. "Na sasa tumeketi pamoja katika mahali pa Mbinguni katika Kristo Yesu." Amina.

125 Hatuna nguvu zozote, bali tuna mamlaka. Haihitaji nguvu. Mtu fulani alisema, "Una nguvu zozote?" La, bali ninayo mamlaka. Hiyo ni kweli.

126 Unachukua polisi mdogo aliyesimama hapa nje. Anavaa sare. Kofia yake ni kubwa sana kwake, inashuka chini hata kwenye masikio yake. Hana nguvu za kusimamisha chochote. Lakini hebu atembee hapa nje, na motokaa inateremka kuja mtaani, ikiwa na injini ya nguvu farasi mia tatu, na hebu ainue huo mkono. Tazama breki zikiteleza. Kwa nini? Yeye hana nguvu zozote, bali ana mamlaka.

127 Na wakati mwanaume au mwanamke amepakwa na ubatizo wa Roho Mtakatifu, huenda asiweze kusoma jina lake katika herufi zenye ukubwa wa behewa, pamoja na elimu, bali yeye—yeye—yeye anayo mamlaka kutoka kwa Mungu, kwamba yeye ni mwana wa Mungu. Acha achukue mamlaka yake, na asimame na kusema, "Simama," na magurudumu ya Shetani yatateleza, na breki zitateleza. Jambo fulani litatukia, kwa sababu amepewa mamlaka na Roho Mtakatifu. "Katika Jina Langu watatoa

pepo." Jambo ndilo hilo. Hakika. Haimbidi kuwa—kuwa na DD.D., ama Ph.D. Inambidi kumjua Yesu, na kujua kile ambacho amepewa. Huyo hapo amesimama. Naam, bwana.

128 Walipaswa wawe wamejua, kwa kutazama kile Mtu huyu alichofanya, na kumkiri Yeye kuwa kile Yeye alichokuwa, Masihi. Basi, Yeye alijua mambo yote, na Yeye alijua shida hii ilikuwa inakuja. Alijua mambo yote. Hakika. "Baba hafanyi chochote isipokuwa Yeye humwonyesha Mwana." Unaona? Kwa hiyo Yeye—Yeye alijua mambo yote. Walipaswa wawe wamejua kwamba Yeye alifahamu kwamba dhoruba hiyo ilikuwa inakuja, vema, na alijua ingetokea. Ilitolewa tu kama jaribu la imani yao.

129 Na labda shida hizi zinafanywa tu, labda uamsho umeisha, kuona kile ambacho tutafanya kuhusu hilo. Labda ugonjwa ulikushika. "Sababu hii, haikuwa dhambi ya mtu yeyote, ila kwamba kazi za Mungu ziweze kufanywa zijulikane." Tunajuaje kuhusu mambo haya, yaliyofanyika? Hakuna jambo linalofanyika, na kawaida tu, si bila ya Mungu kulijua. Yeye analijua. Alilijua, hapo mwanzo. Na mambo haya hufanyika kwa sababu ni jaribio la imani.

130 Petro alisema, "Msione kuwa ni kitu cha kigeni majaribu yanapokuja juu yenu, majaribu makali. Ni bora kwenu kuliko dhahabu. Inafanywa ili kuwathibitisha." Loo, huo moto wa msafisha fedha, kwamba itatokea asilimia mia moja, uchafu wote umeyeyushwa ukatoka, kutokuamini kote, tukio basi, hata unajua! Kile ambacho wana wa Kiebrania wangeweza kushuhudia, baada ya wao kupitia moto, "Mungu ni Mwokozi, kutoka kwenye moto." Walijua hilo.

Danieli alijua, baada ya tukio la tundu la simba.

131 Lazaro alijua, baada ya kaburi, kwamba Yeye alikuwa ndiye ufufuo. Amina.

132 Baada ya wewe kupitia hii mitihani na majaribu, ni matukufu kwako. Ndipo, hili linafanywa kujaribu imani yao. Labda huenda ikawa, usiku wa leo, kwamba baadhi hapa wana ugonjwa, na ni jaribu la imani, kuona kile utakachofanya kuuhusu.

133 Alikuwa amewathibitishia kuwa Yeye alikuwa ni Nani. Alithibitisha kuwa Yeye alikuwa ni Nani. Kwa njia gani? Kwa Maneno ambayo Yeye alihubiri, na kwa kazi ambazo zilifuata Maneno. Unaona? Thibitisho! Mungu alikuwa amemthibitisha Yeye. Kwa kuwa Yeye aliwaambia, "Kama . . ." Alisema, "Kama sizifanyi kazi za Mungu, basi msiniamini Mimi. Kama zile ambazo Mungu alisema nitafanya, kama sizifanyi, basi nihukumuni Mimi, kama sizifanyi. Kama Mimi siye Masihi . . ." Tena, Yeye—Yeye angesema hivyo. "Kama Mimi si Masihi, kama . . . Hamwezi kuniamini Mimi kama Mwanadamu, kuwa Masihi, kwa sababu sikuja kupitia shule zenu, nanyi hamna mahali popote ambapo niliwahi kuelimishwa, ama ambapo

nilipitia shule zenu za theolojia. Na kama hamwezi kuamini kwamba Mimi ndimi Masihi, vema, amininі kazi. Zinashuhudia kile nilicho."

134 Loo, si ingekuwa ajabu, usiku wa leo, kama kanisa lingeweza tu kutulia juu ya hilo, kwamba Biblia ilisema kile Mkristo angefanya na kile angekuwa. Loo, jamani! Jinsi ninavyowazia hilo!

135 Yesu aliwaambia, "Yachunguzeni Maandiko, maana ndani Yake mnadhani mna Uzima wa Milele. Na Hayo ndiyo Ambayo yananishuhudia Mimi. Yanawaambia kile nilicho." Loo!

136 Si lazima niseme mimi ni Mmethodisti, Mbaptisti, Mpresbiteri, ama chochote kile. Maisha unayoishi, Ma—Maneno ya Mungu, kama wewe ni sehemu ya Neno lililo hai, unawezaje kukana kile ulicho? Na Neno linawezaje kukosa kuthibitisha kile ulicho, kama ndivyo ulivyo? Unaona?

137 Inawezekanaje ko—inawezekanaje kondoo aulizwe kutengeneza sufu? Hawezi kutengeneza sufu. Mradi tu yeye ni kondoo, yeye atazalisha sufu kwa sababu yeye ni kondoo.

138 Na mtu hapaswi kutengeneza chochote, kama yeye ni Mkristo. Yeye ni hivyo kwa sababu ndivyo alivyo. Yeye, hilo ndilo ameumbwa kwalo. Yeye ni Mkristo, kiasili.

139 Mti wa tofaa ni mti wa tofaa kwa sababu ni mti wa tofaa. Unaona? Mti wa pichi ni mti wa pichi kwa sababu ni mti wa pichi.

140 Naye Mkristo ni Mkristo kwa sababu Kristo anaishi ndani ya mtu huyo. Na hufanya . . . *Mkristo* inamaanisha "kama-Kristo," si uwanachama; bali, thibitisho, Mungu akizalisha kupitia wewe kile tu Mkristo alicho. Ni wewe kuondoka njiani na kumwacha Mungu aingie ndani, wewe kutochukua mawazo. Acha nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yako. Haya basi. Huyo ndiye Mkristo halisi. Loo, jamani!

"Yachunguzeni Maandiko," Yeye alisema. "Hayo ndiyo Hayo yanayonishuhudia Mimi."

141 Walipaswa wawe wamejua kwamba Yeye alikuwa Mungu aliyeumba upepo na mawimbi. Unaona? Mungu aliumba upepo. Naam. Huo ni hewa. Mungu aliumba maji. Naam. Hiyo ni $H_2O$. Yeye, Yeye aliumba hayo. Bali, unaona, kile kilicho, ibilisi aliingia ndani ya huo upepo, na halafu ibilisi akaja kwenye kitu kingine, akaingia ndani yake, na hiyo ikasababisha dhoruba.

142 Na hivyo ndivyo ilivyo na waaminio wakati mwingine. Wanalegeza kamba, kwa kutokuamini, na halafu Shetani anakuja ndani ya upepo wa kisulisuli, unaona, anasababisha fujo, na wasiwasi, na mabishano, na kila kitu. Huyo ni ibilisi akiingia miongoni mwa watu.

143 Ibilisi huingia miongoni mwa he—hewa na kuizungusha kwelikweli, husababisha mauti; huingia miongoni mwa maji,

huyazungusha kwelikweli. Unaona? Mungu aliyaumba, lakini walimruhusu ibilisi kuingia ndani. Ibilisi aliingia ndani yake, "mkuu wa nguvu za angani." Tazama, aliingia ndani yake, ndipo kukaja upepo na mawimbi.

144 Sasa, wale wanafunzi walipaswa kusema, "Mbona, hakuna shida sasa. Mbona, pale amelala Muumba, amelala papa hapa. Anasafiri pamoja nasi. Unaona? Mbona, hebu angalia tu mambo ambayo Yeye amefanya. Vema, tunajali nini kuhusu mawimbi."

145 Loo, kama tungeweza kujisikia namna hiyo juu yake, jinsi hiyo ingekuwa tofauti. Naam.

146 Mungu, Muumba wa mbingu na—na nchi, Mungu Muumba wa upepo na mawimbi, si ingeyabidi kutii Neno Lake? Jambo pekee Yeye alilopaswa kufanya ni kulinena. Unaona? Yeye ni Neno, lakini Mungu ilibidi amtumie mwanadamu kutimiza, ama kudhihirisha sifa Zake.

147 Mungu, hapo mwanzo, alikuwa Mungu tu. Yeye hata hakuwa Mungu; *Mungu* ni "kitu cha kuabudiwa." Alikuwa ni nguvu kuu, Mungu. Ndipo Yeye akaumba Malaika, nao Malaika wakamwabudu Yeye, kwa hiyo Yeye akawa Mungu. Halafu Yeye akamwumba mwanadamu.

148 Sasa, Yeye ni Mwokozi. Kwa hiyo, hakuna kitu kilichopotea; ilibidi kitu fulani kipotee, ili Yeye aweze kuonyesha sifa Yake kama Mwokozi. Mnaamini hilo?

149 Yeye alikuwa Mponya. Kwa hiyo, hakuna kitu kigonjwa; kwa hiyo ilibidi kuwe na kitu kinachoumwa, kudhihirisha sifa Yake, kuonyesha kwamba Yeye alikuwa.

150 Alikuwa Baba, unaona, na kitu fulani ilibidi kiwe. Ilimbidi kuwa na Mwana, kumfanya Yeye Baba. Unaona?

151 Na vitu hivi vyote vikionyesha sifa Zake, hakuna kitu nje ya utaratibu. Unaona? Kuna . . . Mungu anafanya kila gurudumu liende sawa tu kabisa. Kila kitu kiko sawa. Muumbaji, haleluya, Muumba yuko ndani ya chombo ambacho tunasafiria.

152 "Ingawa mabuu ya ngozi wanauharibu mwili huu, hata hivyo katika mwili wangu nitamwona Mungu, Ambaye nitamwona mwenyewe," kasema Ayubu. Hiyo ni kweli. Daudi alisema, "Naam, nijapotembea kupitia bonde la kivuli cha mauti, sitaogopa uovu wowote, kwa kuwa Wewe uko pamoja nami. Hata nikifanya kitanda changu kuzimuni, Yeye yuko huko. Hata nikichukua mabawa ya asubuhi na kuruka na kutoweka, Yeye yuko huko." Kusafiri kwenye bahari kuu ya maisha!

> Na maisha ya watu mashuhuri yote hutukumbusha
> Tunaweza kufanya maisha yetu kutukuka,
> Pamoja na kuachana, huacha nyuma yetu
> Nyayo, (kama *hii*) kwenye mchanga wa wakati;
>
> Nyayo, ambazo labda mwingine,

Huku akisafiri kwenye bahari kuu ya maisha,
Ndugu mpweke ambaye chombo kimemwendea mrama,
Katika kuona, atatiwa moyo tena.

"Kama Mungu alimfanyia vile ndugu yule, Yeye atanifanyia mimi."

Hebu tuamke na kufanya basi,
Kwa moyo kwa ajili ya vita vyovyote; (Hilo ndilo ningeninii . . .)
Msiwe kama ng'ombe bubu, wanaokimbizwa! (Ambao lazima wakimbizwe ili kuingia katika chochote.)
Hebu tuamini, tuwe shujaa katika vita!

153 *Zaburi Ya Maisha*, Shairi la Longfellow, *Zaburi Ya Maisha*. Ninalipenda. Linaeleza jambo fulani. Linadhihirisha jambo fulani. Lina kitu fulani halisi ndani yake, maana fulani. Ninapenda kitu kilicho na rangi ndani yake, kina maana. Muziki, shairi, chochote kiwezacho kuwa, ninakipenda kama ni halisi.

154 Sasa, walipaswa wawe wamejua Yeye ingembidi, kila kitu ilibidi kimtii Yeye. Tunapaswa kujua jambo lilo hilo. Miili yetu itabidi itii Neno Lake. "Mimi ndimi Bwana aponyaye magonjwa yako yote." Je! hilo ni Neno? Vema, mwili huu lazima utii hilo.

155 Yote yanayonipasa kufanya ni kubonyeza kitufe. Amina. Wakati mwingine kitufe kiko magotini, mwajua. Ila, nawaambia, hicho hufanya umeme kupita.

156 Lakini hayo ndiyo yote unayofanya ni kuamini hilo. Mungu aliliahidi. Na jinsi yale mawimbi ilibidi yamtii Yeye, ndivyo na *hii* haina budi kumtii Yeye. Kiasi kwamba, Yeye aliahidi, baada ya sisi kuangamia, "Nitamfufua tena, kwenye siku ya mwisho."

157 Nilikuwa nikichana nywele hizi mbili ama tatu nilizo nazo, hapa si muda mrefu uliopita. Ndipo mke wangu akaniambia, ameketi huko nyuma, alisema, "Billy, unaingia kipara."

158 Nikasema, "Lakini, unajua, mpenzi, sijapoteza hata moja ya hizo."

Akasema, "Ati nini? Hujapoteza moja ya hizo?"

Nikasema, "La."

Akasema, "Naomba uniambie mahali zilipo."

159 Nikasema, "Basi ninataka kukuuliza kitu. Wewe niambie mahali zilipokuwa kabla sijazipokea. Hizo ni bayana. Na mahali zilipokuwa kabla sijazipata, ziko huko zinaningojea kuziendea." Kweli.

160 Alisema, "Hakuna hata unywele mmoja wa kichwa chako utakaoangamia." Hakuna kitakachoangamia. Je! unajua wewe . . .

161 Kitu cha uharibifu kuliko vyote tulicho nacho ni moto. Bali moto haungamizi. Huteketeza tu asidi na oksijeni mpaka inarudi moja kwa moja kwenye kile ilichokuwa hapo kabla. Mungu haangamizi chochote. Huwezi kuangamiza kabisa kitu chochote. Haleluya! Kweli. Huwezi kuangamiza chochote. Kitarudi kwenye asili yake.

162 Mimi hutia risasi kwa mkono. Ninafyatua Swift .220, na ninaiweka futi elfu tano kwa sekunde kwenye mrututu. Na halafu unaweka tu nusu ya wakia wa baruti ndani yake, na unapiga risasi kwenye ukuta pale, huoni chochote. Haitafanya doa. Yote unayosikia ni kelele. Kunafanyika nini? Wakati risasi inapotoka kwenye mtutu upesi sana pamoja na hiyo shaba nyekundu na risasi, mpaka inageuka kurudi kwenye asidi zake za asili, kabla haijakuwa, miaka milioni mia moja iliyopita, labda. Lakini kama ulimwengu ungesimama muda huo wote, huenda ikarudi tena kuwa risasi, tena. Unaona, hiyo, hakuna kitu kinachoangamizwa. Kinarudi nyuma. Loo, ni kitu cha ajabu jinsi gani!

163 Ninawaweka muda mrefu kupita kiasi. Vema. Nitafunga, kidogo tu. Unaona?

164 Sasa, Mungu alisema, “Nitaufufua tena katika siku za mwisho.” Ajabu jinsi gani!

165 Walipaswa kujua hili. Walipaswa kuwa wamejua Yeye angefanya upepo na mawimbi kumtii Yeye, baada ya wanafunzi Wake kujikuta kwenye mwisho wa uwezo wao.

166 Ee Mungu, jalia tufanye jambo lilo hilo, usiku wa leo, tuone juhudi zetu za kibinadamu kwenye mwisho.

167 Walipojikuta, hapana shaka iliwafunukia kwamba Muumba alikuwa pamoja nao; baada ya da—daktari wao kushindwa, baada ya mapokezi yao yote ya Kristo kisaikolojia kushindwa, baada ya madaktari kushindwa, na kila kitu.

168 Kumbukeni tu kwamba Muumba yu pamoja nasi. Mnaona? Yeye yupo hapa, Yule Ambaye aliahidi mambo haya. Waebrania 13:8.

Ndipo kukaja wazo, “Hebu twendeni, tukamwamshe Yesu.”

169 Hiyo ndiyo hatua inayofuata. Hilo ndilo jambo kwa ajili yetu. Hebu twende, tumwite Yeye jukwaani. Aliahidi kuwa pamoja nasi. Si Yeye aliahidi? “Tazama, niko pamoja nanyi daima, hata mwisho wa ulimwengu.” “Yesu Kristo yeye yule jana, leo, na hata milele.” Nenda, kamwamshe Yesu, kwa kuwa Yeye yuko pamoja nasi, kama Yeye alivyokuwa wakati ule.

170 Walikuwa wameliona Neno la Kimaandiko la Mungu likithibitishwa, kwamba huyo alikuwa ndiye Masihi. Walilijua. Unaona? Vivyo hivyo na sisi. Tumeona kitu kile kile, ambacho kilikuja kwenye Siku ya Pentekoste, kikija moja kwa moja juu yetu; maagizo yale yale, jambo lile lile likifanyika. Tulimwona

Yesu akisimama moja kwa moja miongoni mwetu, akifanya kazi kupitia watu, na kuwaponya wagonjwa, na kuwafufua wafu, na kufungua macho yaliyopofuka, na kufanya kazi zile zile Yeye alizofanya wakati ule, sawa tu na alivyoahidi Yeye. Kwa hiyo hakupaswi kuwa na mahangaiko yoyote kuhusu hilo. Unaona? Sasa, hatupaswi kuwazia juu yake.

171 Mwanamke fulani wakati mmoja aliniambia. Wakati nikihubiri, ilitokea kwamba niliwaza juu ya hili. Kulikuwa na mama fulani aliyeniambia, alisema, "Ndugu Branham." Nimetaja hili, mara nyingi, lakini huenda ikafaa kulisema tena. Alisema, "Kuna kitu kimoja tu ninachoona kasoro katika mahubiri yako."

172 Nikasema, "Loo, jamani, asante, unaona, 'kitu kimoja tu'" nikasema, "Kwa—kwa hakika ninakushukuru."

173 Alikuwa ni mfuasi wa kanisa ambalo halikuamini kwamba Yesu alikuwa Mungu. Hakuamini kwamba Yeye alikuwa wa kimbinguni. Hawakuamini. Hakuamini kwamba—kwamba Yeye alikuwa kile Yeye alichokuwa, Masihi. Alisema, "Alikuwa Nabii. Alikuwa Mtu mwema, lakini Yeye asingeweza kuwa Mwana wa Mungu. Maana, Mungu asingaliweza kuwa na Mwana. Mungu ni Roho." Unaona? Alikosa kuelewa kwamba Mungu alimtia uvuli Mariamu, ambalo lilileta kuzaliwa na bikira. Unaona? Ndipo akaniambia, "Unamfanya Yeye kuwa Mungu, Bw. Branham."

Nikasema, "Yeye ni Mungu."

174 Akasema, "Mbona," kasema, "mbona, Yeye asingeweza kuwa Mungu." Kasema, "Wewe ulisema unaamini Biblia."

Nikasema, "Ninaamini."

175 Akasema, "Kama nitakuthibitishia, kwa Biblia yako mwenyewe, kwamba Yeye hawezi kuwa Mungu, kwamba Yeye alikuwa Mwanadamu tu, Mtu mwema." Na wao, vema, kama kuna mmoja wao hapa ndani, sitaki kuumiza hisia zako. Maana, Kristo alikufa. . . Ilikuwa ni Sayansi ya Kikristo, unaona. Tena kasema, "Sasa, uponyaji wako na kadhalika," kasema, "Ni—ninaamini huo, kila sehemu, lakini," akasema, "wewe unamfanya Yesu kuwa Mungu."

176 "Mbona," nikasema, "Yeye ama ni Mungu au mdanganyifu mkubwa kuliko wote ulimwengu uliwahi kuwa naye." Unaona? Nikasema, "Yeye ama alikuwa Mungu au Yeye hakuwa chochote." Unaona?

177 Ndipo akasema, "Loo, jamani, Bw. Branham!" Kasema, "Asingeweza kuwa Mungu."

Nikasema, "Vema, nipe Andiko lako."

178 Akasema, "Wakati Yeye alipokuwa akishuka kwenda kwenye kaburi la Lazaro, katika Yohana Mtakatifu mlango wa 11," kasema, "Biblia ilisema Yeye alienda huko chini kwenye kaburi la Lazaro."

Kasema, “Naam, mama. Ninajua mahali unaposoma.”

179 Akasema, “Halafu Biblia ilisema, ‘Njiani Mwake akienda huko chini, kwamba Yeye alilia.’”

Nikasema, “Hiyo ni kweli.”

Akasema, “Vema, angewezaje Yeye kuwa Mungu, na halafu alie?”

180 Nikasema, “Vema, unakosa kuona kile Yeye alichokuwa. Yeye alikuwa Mwanadamu na Mungu pia.” Unaona? Nikasema, “Alikuwa Mwanadamu wakati Yeye alipokuwa analia. Hiyo ni kweli. Bali wakati Yeye aliposimama kando ya kaburi la mtu huyo aliyekuwa amekufa, siku nne, na kusema, ‘Lazaro, njoo huku.’ na mtu aliyekuwa amekufa, siku nne, akafufuka na kutoka kaburini, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu.” Kweli.

181 Nikasema, “Kweli, Yeye alikuwa Mwanadamu wakati Yeye aliposhuka kutoka mlimani usiku ule, njaa, na akaangalia kote kwenye m—mtini, kupata kitu cha kula. Alikuwa Mwanadamu wakati Yeye alipokuwa na njaa. Lakini wakati Yeye alipochukua biskuti tano na samaki wawili, na kulisha watu elfu tano, huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu.” Kweli. Ni kweli.

182 Tena nikasema, “Alikuwa mwanadamu wakati Yeye alipokuwa amelala nyuma ya chombo, amechoka, mahali ambapo hata mawimbi hayakuninii. . .hata hayakumwamsha Yeye, kuonekana kumwamsha Yeye. Alikuwa Mwanadamu. Hapana shaka kwamba pepo elfu kumi wa baharini walikuwa wameapa wangemzamisha Yeye usiku huo. Unaona? Sasa, Yeye alikuwa Mwanadamu amelala pale, amechoka. Bali wakati mara alipoitwa jukwaani, amina, Yeye aliweka mguu Wake demani mwa chombo, akatazama juu na kusema, ‘Amani,’ akatazama chini kwenye mawimbi na kusema, ‘Tulia,’ na upepo na mawimbi yakamtii Yeye. Amina. Huyo alikuwa zaidi ya mwanadamu.” Naam, bwana.

183 Alikuwa ni Mwanadamu msalabani, wakati Yeye alipolia kwa ajili ya maji ya kunywa. Alikuwa ni mwanadamu akilia, “Ninaona kiu.” Lakini kwenye asubuhi ya Pasaka, wakati Yeye alipovunja mihuri ya mauti, kuzimu, na kaburi, na kupaa juu, Yeye alikuwa zaidi ya Mwanadamu. Huyo alikuwa Mungu ndani ya Mwanadamu. Hiyo ni kweli.

184 Na yuyo Huyo anaishi ndani yetu, usiku wa leo, kama Nafsi ya Roho Mtakatifu. Naam, bwana.

185 Watu leo hii wanasema, “Ningewezaje kuamini kwamba Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele?” Kumbukeni, Yeye aliahidi, katika Kitabu cha—cha Waebrania, kwamba, “Yeye alikuwa ni yule yule jana, leo, na hata milele.”

186 Aliahidi, pia, katika Ki—Kitabu cha Yohana Mtakatifu, mlango wa 14 wa Yohana Mtakatifu, na kifungu cha 12, Yeye alisema, “Aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo yeye atazifanya

pia. Mambo ambayo ninaishi, ambayo Baba anaishi ndani Yangu, Mimi nikiwa Mwana wa Mungu; ninapowafanya wana, Roho Yangu itakuwa ndani yenu na kufanya mambo yayo hayo." Hakika. Hilo ni kawaida tu.

187 Tena, Yeye alisema, "Tazameni, niko pamoja nanyi daima, hata mpaka mwisho wa ulimwengu." Mathayo 28, 28:22, ama 28:20, ndivyo ilivyo. "Tazama, Mimi pamoja nanyi daima, hata mwisho wa ulimwengu. Niko pamoja nanyi. Kitambo kidogo," Yeye alisema tena, "na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi. Kwa kuwa Mimi. . . " *Mimi* ni kiwakilishi kingine cha nafsi. Unaona? "Nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa ulimwengu. Kazi nizifanyazo mtazifanya pia." Haya basi. Hivyo hasa ndivyo ambavyo ungelijua. Loo, tena, "Sitakuacha kamwe wala sitakupungukia."

Unasema, "Hiyo inawezaje kuwa? Inaweza kuthibitishwa kwa njia gani?"

188 Yohana 14:12, unaona, "Kazi nizifanyazo nanyi mtazifanya pia." Yeye sasa anangojea kuitwa jukwaani. Anangojea kwenye saa hii hivi sasa, kuthibitisha hasa kile ambacho nilisema juu Yake, kuwa hivyo sasa hivi. Kama sivyo, basi *Hii* ni uwongo na mimi ni shahidi wa uwongo. Yeye yuko tayari kuitwa jukwaani sasa hivi, kufanya mambo yale yale aliyofanya Yeye.

189 Kwa hiyo katika chombo ambacho tunasafiria, hebu tumwamshe Yesu katika maisha yetu. Sikilizeni. Nimesema mara kwa mara. Kama nilisimama hapa jukwaani na kuwaambieni kwamba roho ya John Dillinger iliishi ndani yangu, mbona, ningekuwa na bunduki na kuwa haini. Hakika. Kama niliwaambia kwamba—kwamba—kwamba Shakespeare aliishi ndani yangu, ningalikuwa mshairi. Kama huyo Shakespeare aliishi ndani yako, mbona, wewe, ungalijua jinsi ya ku. . . Ungekuwa ndiye mtunzi mashuhuri wa washairi. Hiyo ni kweli? Hakika. Ungeweza. Mashairi, ungetunga mashairi, kwa sababu Shakespeare, m—mtunzi mashuhuri, angekuwa ndani yako, na wewe ungekuwa ni Shakespeare. Je! hiyo ni kweli? Kama Shakespeare aliishi ndani yako, si ungekuwa Shakespeare? Hakika, ungekuwa.

190 Kama Beethoven aliishi ndani yako, si ungekuwa mtunzi wa nyimbo, mtunzi mashuhuri, Beethoven? Unasema, "Beethoven anaishi ndani yangu." Basi utafanya kazi za Beethoven. Utaandika nyimbo zake, hakika, kama uliishi ndani yako. Bila shaka ungefanya hivyo, kwa sababu kwamba roho yake iliishi ndani yako.

191 Basi, kama Kristo anaishi ndani yangu, kama Kristo anaishi ndani yangu, kazi za Kristo zitafanywa kupitia mimi. Hakika. Kama Beethoven anaishi ndani yako, kazi za Beethoven zitafanya ijulikane. Kama Kristo aliishi ndani yako, kazi za

Kristo zitafanywa zijulikane, kwani Yeye ni yule yule. "Yule yule," Yeye hawezi kubadilika. Mnakumbuka kile nilichosema? Ni cha Milele. Yeye hawezi kubadilika. Ni yeye yule jana, leo, na hata milele.

192 Loo, basi, mwite Yeye jukwaani. Je! unaogopa kumwita? Je! watu wa saa hii, je! watu wa siku hii, wanaogopa kumwita Yesu jukwaani, kusema, "Bwana, Wewe uliahidi hilo. Sasa lifanye"? Loo, jamani.

[Dada fulani ananukuu Zaburi 103:1-9, 11—Mh.] Amina. Zaburi.

193 Yehova ni mkuu! Loo, mwenye nguvu ni Yehova! Wa milele ni Yehova. Yeye ni kuanzia milele hadi milele. Yeye ni Mungu. Rehema Zake hudumu kwa maelfu ya vizazi, ziko juu ya wale wanaomcha Yeye.

194 Je! unaogopa kumwamsha huyo Yesu maishani mwako, ambaye amekuwa akilala kwa muda? Je! unaogopa kuamsha kitu hicho ambacho, miaka michache iliyopita, kilikuwa kimeshuka juu yako na kukujaza na baraka Zake? Je! unaogopa kumwamsha Yeye, na kusema, "Bwana Yesu, niko taabuni, usiku wa leo. Tembea jukwaani kwa ajili yangu. Katika kusafiri baharini, nimeshikwa na ugonjwa. Ninateseka. Nisaidie, Ee Bwana Mungu. Nisaidie"? Hivi unaogopa kumwita Yeye jukwaani? La.

195 Wakati ukimwita Yeye jukwaani, kama wale wanafunzi, shaka lote hujitwalia kiti chake, huketi chini. Imani huinuka. Mashaka hayapo tena. Imani imechukua nafasi.

Imeandikwa katika Biblia, kwamba, Waebrania 13:8, ilisema, "Yesu Kristo ni yeye yule jana, leo, na hata milele." Imeandikwa, sasa na ifanyike.

196 Imeandikwa katika Yohana Mtakatifu 14:12, kama ambavyo ndio kwanza ninukuu hapa, "Yeye aniaminiye Mimi, kazi nizifanyazo Mimi yeye atazifanya pia." Je! hiyo ni kweli? Lakini imeandikwa, sasa hebu ifanyike. Unaona? Mungu aliahidi hiyo. Mungu alisema hivyo.

197 Imeandikwa, Mathayo 28:20, "Tazama, niko pamoja nanyi daima, hata kufikia mwisho wa ulimwengu." Unaona? "Kitambo kidogo na ulimwengu hautaniona Mimi tena, hata hivyo nyinyi mtaniona Mimi; kwa kuwa nitakuwa pamoja nanyi, hata ndani yenu, hadi mwisho wa wakati." Hiyo imeandikwa, "Nyinyi mtaniona Mimi." Imeshaandikwa, sasa hebu ifanyike. Mnaamini hilo?

198 Nimewaweka kuchelewa. Ni saa tatu u nusu. Na ninajua pengine mngekuwa mmeenda nyumbani na tayari mmeenda kulala kufikia wakati huu. Ngojeni tu kidogo. Mambo haya, nina yapata dazani moja zaidi ya muhtasari hapo, bali sitauendea.

199 Tazama. Je! mambo haya ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Kama si kweli, basi tunafanya nini hapa? Tunadai nini, kitu fulani, hata tunakuwa wanafiki? Tunadai nini, kwa ulimwengu, mambo ambayo—ambayo hata hayako hivyo? Mbona, tunapatikana tukiwa mashahidi wa uwongo, na hata hatupaswi kuruhusiwa kuishi. "Basi ikiwa hakuna ufufuo wa wafu, na Kristo hajafufuka kutoka kwa wafu, basi kuleni, mnywe, na mfurahi." Nyinyi nyote tokeni nje mkaishi kama takataka nyingine, pamoja na nguruwe, mnaona, kama hakuna ufufuo. Kama hakuna kuja kwa Kristo, kama kuna . . . kama—kama Yeye hayupo hapa, na Maneno Yake si kweli, kama yodi moja si kweli, basi siwezi kuwa na imani katika yoyote ya Hilo. Halina budi kuandikwa lote, lote halina budi kuwa sahihi.

200 Hii ndiyo saa, ambapo Yesu alisema, "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa kwenye kuja kwa Mwana wa Adamu." Tazama, tazama Sodoma, kwa dakika moja tu, kama kufunga. Huko Sodoma, kabla, ulimwengu uliteketezwa, ulimwengu wa Mataifa uliteketezwa. Sasa, wakati huu, unaenda kuteketezwa tena. Unaona? Si maji tena; moto, wakati huu. "Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma." Sasa, tazama ha—hali ya ulimwengu leo, kama tu Sodoma, wakivalia tu namna ile ile, kila kitu. Ninawaambieni. Ni aibu. Pia angalia ulimwengu, unazagaa tu katika dhambi.

201 Tazama, hata, limeingia ndani ya kanisa. Na Mkristo wa mtindo wa kale, hatuwaoni, kabisa, tena. Na wa—wanawake wetu, wote wamekata nywele zao, wanajipaka vipodozi, wanavaa kaptura, na—na kila kitu, kizinifu kabisa, na bila kujua kwamba mnaenda kuulizwa kwenye Siku ile kutoa jibu kwa ajili ya uzinzi. "Yeyote amtazamaye mwanamke kwa kumtamani amezini naye tayari." Huenda ukawa safi, mwenye sifa, namna hiyo. Lakini vile umefanya, na wenye dhambi wanakutazama, njia mbaya. Ulijianika mwenyewe, basi una hatia. Una hatia. Yesu alisema hivyo. Waangalie hata wanawake wetu wa Kipentekoste.

202 Pia waangalie wahudumu wetu, wengi wao hulegeza, wanaogopa kusema chochote dhidi yake, wanahofia kwamba shirika la kimadhehebu litawatupa nje.

203 Afadhali nilale njaa, na kunywa maji ya matawi na kula biskuti kavu, na kuhubiri Neno hilo na kusema Kweli, naam, bwana, kuliko kuwa mshiriki wa kila kitu kilichoko. Naam, bwana.

204 Loo, tunahitaji kilindi cha unyofu. Tunahitaji kitu fulani kirudi. Hatuhitaji maonyesho mengi. Tunahitaji Roho Mtakatifu aishi miongoni mwetu, kufikia mahali ambapo watu wanaweza kusema, "Ni nani awezaye kunishtaki kwamba nina dhambi?" Dhambi ni kutokuamini.

205 Kama Maandiko yalisema kwamba Yesu atafanya fulani-na-fulani, Yeye alisema, "Ni nani kati yenu awezaye kunihukumu Mimi, ama kunishtaki Mimi kuwa nina dhambi?"

206 Sasa, ipo dhambi moja tu, hiyo ni kutokuamini. Hiyo ni, imani au kutokuamini. "Yeye asiyeamini amehukumiwa tayari." Unaweza kuvuta sigara, kunywa vileo, na kufanya mambo haya kwa sababu huamini. Lakini kama unaamini, utafanya tofauti. Unaona? Ni kwa sababu ama imani au kutokuamini kuko ndani yako.

207 Sasa, tazama. Kaa kimya kwa dakika moja. Sasa, hili hapa tamko kubwa mashuhuri. Ninaangalia juu ya kusanyiko hili, kwanza. Ninaangalia kote.

208 Na ni—ni—ninamjua mtu mmoja ambaye ninaweza kumwona pale nje, ambaye si—sijui kwamba ninamjua. Ni mwanamume ambaye—ambaye nilimsimamisha hivi majuzi. Sikujua. Basi lilikuwa linajaribu kupiga kona kushoto, na watu wakipiga kona. Nikawaza, "Jamaa yule anajaribu kugeuka, kushoto." Nikasimama, nikamwashiria kuendelea kugeuka. Na kuna dereva wa basi anayeketi hapa. Na huyo ni. . .na hapa. Nilikutana na yeye kwenye mkahawa wa Furr leo, ama hoteli, na yeye akaniambia alikuwa ndiye mwanamume huyo. Kasema mke wake alikuwa ameponywa katika mmoja wa mikutano mahali fulani akiwa na ugonjwa wa figo, mafigo yanayoelea ama kitu fulani, na kutajwa, katika mkutano. Unaona? Mimi kamwe. . .Mungu Mbinguni anajua kamwe sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Sijawahi kumwona. Naye huyu hapa mwanamume huyo. Nadhani, mke wake, ninaamini yupo hapa mahali fulani, itakuwa ushuhuda. Mnaona? Na mambo, yanaendelea tu na kuendelea. Mnaona?

Na mimi sioni mtu yeyote ambaye kwa hakika ninamjua.

209 Bali, kumbukeni, Mungu anajua kila mmoja wenu. Anajua kilichoko moyoni mwako. Na kama Yeye ni Neno. . .Mnaamini Yeye ni Neno? Biblia ilisema, "Neno la Mungu lina nguvu, ni kali kuliko upanga ukatao kuwili, Mtambuzi wa mawazo ya moyoni." Je! hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo sababu Yesu angeweza kusimama na kutambua mawazo yao, na kuwaambia kile walichokuwa wamefanya. Mnaona? Hiyo ni kweli.

210 Yule mwanamke aligusa vazi Lake. Ndipo Yeye akageuka, kasema, "Ni nani aliyenigusa?" Hakujua kwenye wakati huo. Na kila mtu alikana hilo.

211 Lakini aliangalia kote, mpaka Yeye akapata mahali nguvu hizo zilikuwa zimeenda. Aliziona juu ya maskini mwanamke. Ndipo Yeye akamwambia mwanamke huyo kuhusu kutokwa kwake na damu, tena kasema, kwamba, "Imani yako imekuokoa." "Imani yako." Alikuwa amevuta kupitia Mungu, akavuta kutoka kwa Mungu, kupitia Yeye. Hiyo ndiyo sababu

nguvu zilikuwa zimetoka, uweza. Imani ya mwanamke huyo ilikuwa imemgusa Mungu, kupitia Yeye. Unaona?

212 Sasa, "Kazi nizifanyazo nyinyi pia mtazifanya." Mnaona ninachomaanisha?

213 Mtu fulani alisema, "Loo, tunafanya kazi kubwa zaidi." Vema, zifanye tu kazi, kwanza, unaona. Na ufanye tu kazi. Unaona?

214 Unasema, "Tunahubiri Injili kote ulimwenguni. Hiyo ni kubwa." Unajaribu kujificha nyuma ya kitu fulani, jamani. Unaona?

215 "Kazi nizifanyazo, pia. Kazi nizifanyazo nyinyi pia mtazifanya; na nyingi kuliko hizi, kwa kuwa ninaenda kwa Baba." Mnaona?

216 Mwangalie yule mwanamke kisimani, na kadhalika. Hivyo ndivyo walivyojua Yeye alikuwa Masihi. Kama Yeye angalikuja usiku wa leo, kwenye jiji, mngejuaje ilikuwa ni Yeye? Unaona? Makovu ya msumari, mnafiki yeyote anaweza kufanya hilo, kuweka kovu la msumari kwenye mkono wake, unaona, chochote. La, bwana. Njia pekee wanayopata kuijua, ni utambulisho wa Roho, unaona, atafanya kazi ambazo Yeye alisema Huyo atafanya. Sasa, ninaamini hilo.

217 Ni kwa nini niko na kundi hili la watu wa Kipentekoste? Mimi si mfuasi wa lolote la madhehebu yao, kwa sababu ninasimama tu katika pengo na kusema, "Sisi ni ndugu," yote ya hayo. Unaona? Kwa sababu ninaamini wana kitu kilicho karibu sana na kile ninachofikiria Biblia ilicho, kwa mtu yeyote nimjuaye. Mnaona? Hiyo—hiyo ndiyo sababu ninafanya hivyo. Sijiungi kamwe, maana ninawaona pande zote mbili, ndugu walio na Roho Mtakatifu. Ninaamini hilo. Ninajua ni kweli. Unaona? Basi kwa hiyo sipendi kujenga juu ya *hili* moja, ama kujenga juu ya *lile* moja, ama kuondoa kwenye *hili* na *lile*. Ninasimama tu na kusema, "Sisi ni ndugu." Sahauni tu kuhusu *hayo*. Hebu tuwe ndugu, mnaona. Hebu tuwe tu ndugu. Na mradi tu Shetani ametufanya tupigane mmoja na mwenzake, mbona, haimbidi yeye kupiga vita hata kidogo. Lakini mradi tu tunasahau vita hivyo, na kuunganisha mikono na mioyo, na kusema, "Sisi ni ndugu," tunasonga mbele, askari Wakristo, halafu, uamsho huo mkubwa. Hakuna baraza lolote la ekumeni litakalowahi kugusa hilo. La, bwana. Hilo ndilo chaguo la Mungu, Mteule aliyeitwa, sasa. Ikiwa siku . . .

218 Kumbukeni tu, ishara ya mwisho iliyofanywa, kabla ya Sodoma kuteketezwa, ilikuwa ni Mungu akidhihirika katika mwili wa mwanadamu. Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Ninauliza hilo. Malaika watatu walimjia Ibrahimu.

219 Na wawili kati ya Malaika hao wakashuka kwenda huko chini Sodoma, kutoa onyo. Hilo lilikuwa kwa ajili ya walio

vuguvugu, kanisa la kimadhehebu, Billy Graham wa kisasa, na kadhalika.

220 Bali Ibrahimu aliwakilisha, kama ilivyokuwa katika siku hiyo, Kanisa teule ambalo halikuwa huko chini Sodoma. Liko nje ya Sodoma, wapentekoste halisi waliozaliwa upya na wote ambao wamezaliwa kwa Roho. Sasa mwangalie Yule aliyebaki nyuma na kuongea na Ibrahimu. Kasema . . .

221 Sasa kumbukeni, jina lake lilikuwa Abramu, siku chache kabla ya hapo, naye Sarah alikuwa S-a-r-r-a. Na lilikuwa limebadilishwa kuwa Abraham, na kuwa S-a-r-a-h, Sarah. Unaona? A-b-r-a-h-a-m, *Abraham*, "baba wa mataifa." Unaona?

222 Na si linashangaza, kwamba, watu wote mashuhuri ambao wamewahi kuenda kwenye kanisa la Sodoma huko nje, ulimwenguni leo, watu wote mashuhuri ambao waliwahi kuenda huko nje. Kumekuwa na Billy Sunday, Sankey, Finney, Knox, Calvin, Luther, kadhalika. Hakuna hata mmoja wao aliyekuwa na jina lililoishia na h-a-m, mpaka leo, G-r-a-h-a-m. Hakuna mwingine, wakati wowote. Hilo ni herufi sita. Ambapo, Abraham ni A-b-r-a-h-a-m, saba, kamilifu. Unaona? Bali angalia. Malaika aliyemjia Ibrahimu, alimwambia, "Abraham," si Abram. "Ibrahimu, yu wapi mkeo," sio Sarra, bali, "Sarah."

Na Biblia ilisema, "Yuko hemani nyuma Yako."

223 Ndipo Yeye akasema, "Mimi . . . " Haya basi, kiwakilishi cha nafsi tena. "Ninaenda kukuzuru, Ibrahimu," kulingana na ahadi ambayo Yeye alitoa.

224 Huyo alikuwa ni nani? Vumbi kwenye nguo Zake. Akala ndama, akanywa maziwa kutoka kwa ng'ombe, akala siagi, mkate. Ameketi pale, alifanya kama Yeye alijaa mavumbi na amechoka. Hebu . . . Akaosha miguu Yake, Mwanadamu, alivyoonekana. Ndipo Yeye akasema, "Yu wapi Sarah?"

Kasema, "Yuko hemani, nyuma."

"Nitakuzuru, kulingana na . . . "

225 Na yeye alikuwa, kile mnachokiita, anadukiza, mwajua, akisikiliza kupitia hema. Hakukimbia nje kama wanawake leo hii, mwajua, na inawabidi kufanya hivyo, mwajua. Bali, yeye, anasikiliza kupitia hema, kile mume wake alikuwa anasema. Siku hizi, mke husema kile mume anapaswa kusema. Kwa hiyo basi alisikiliza namna hiyo, kupitia hema. Ndipo wakati aliposikia . . . Si nyinyi kina dada, la, la; mnajua bora kuliko hapo. Unaona? Lakini, vema, alikuwa anasikiliza.

226 Na yeye—yeye akacheka, kifichifichi, kasema, "Mimi, mwanamke mkongwe, mwenye umri wa miaka mia moja, na bwana wangu, pia mkongwe, na ati tuwe na raha tena?" Unaona, kama mume na mke, walikuwa wamekoma, miaka na miaka hapo kabla. "Mimi niwe na raha na mume wangu tena, sisi tuwe na raha pamoja?" Ndipo akacheka.

227 Naye Malaika, huku ninii Yake. . .Mtu huyo, huku mgongo Wake umeelekea kwenye hema, kasema, “Ni kwa nini Sara akacheka?”

Naye akasema, alitoka nje mbio na kukiri, “Sikusema.”

“Lakini ulisema.” Unaona?

228 Sasa, Mungu angalichukua uhai wake pale pale. Lakini asingaliweza kumdhuru, kwa kuwa yeye ni sehemu ya Ibrahimu. Loo, tungekuwa tumeondoka kitambo sana, kama haikuwa sehemu ya Kristo. Mambo yote ambayo Yeye amefanya, na sisi tumezunguka na kusema, “Ni kuwasiliana kiakili. Ni *hiki*, *kile*, ama *kinginecho*.” Bali Yeye hawezi kukugusa. Unaona? Ghadhabu haiwezi kukugusa, kwa sababu wewe ni sehemu ya Kristo wakati unapozaliwa mara ya pili. Unaona? Unaona? Asingeweza kufanya, hiyo kwa sababu ingemdhuru Ibrahimu. Ahadi Yake ilikuwa kwa Ibrahimu, na Sara ni sehemu ya Ibrahimu. Nalo Kanisa ni sehemu ya Kristo, Bibi-Arusi. Unaona? Asingeweza kulifanya, ingawa kutokuamini kwake.

Alisema, “Lakini ulifanya.”

229 Biblia ilisema yeye mke alikuwa anaogopa. Labda alikuwa anaogopa kuwa angepoteza uanachama wake au kitu fulani, bali, unaona, unaona, kama leo hii. Bali—bali alikuwa ameogopa.

230 Basi, tazama, Mtu yuyo huyo alimpa Ibrahimu baraka. Na ahadi, kwamba, kama angeweza kupata nafsi kumi zenye haki, Yeye asingeiharibu, na akatoweka mbele zake.

231 Ndipo Ibrahimu akamwita *Elohimu,* “Yule anayejitosheleza kwa yote.” Sasa chukua Biblia yako na uangalie. Kama. . . “Hapo mwanzo Mungu. . . ” Angalia kama huyo si “Elohimu.” Na hapa Ibrahimu, ambaye alizungumza na Yeye, akayaita madhihirisho haya Mtu hapa, kabla tu ya kuteketezwa kwa Sodoma, ambaye aliweza kutambua mawazo yaliyoko niani, kasema ilikuwa ni “Elohimu.”

232 Na Yesu alisema, “Kama ilivyokuwa katika siku za Sodoma, ndivyo itakavyokuwa.” Sasa angalia yule ambaye ameenda kwenye kanisa, dhehebu. Tazama kile Mungu anachofanya miongoni mwa Wateule. Hapo tu ni ishara ya mwisho ambayo Ibrahimu alipokea, Ka—Kanisa lililoitwa litoke, lilipokea kabla ya Sodoma kuteketea. Tuko katika siku za mwisho.

233 Marafiki, mwamsheni Yesu. “Bwana, Wewe ulitoa ahadi.” Usiogope. Sema, “Bwana Mungu, kwa ujasiri ninachukua hatua. Ninajiamsha, hapa ndani. Amka, Bwana, kwa kilio changu. Nina haja. Nirehemu. Nimekosa kuamini, na unisamehe kwa ajili ya hiyo. Nijalie, tangu sasa, ninataka kukuita Wewe jukwaani, kwa ajili ya hali yangu.”

234 Biblia ilisema, “Yeye ni Kuhani Mkuu awezaye kuguswa na mambo ya udhaifu wetu.” Je! hiyo ni kweli? Agano Jipya,

Waebrania 1, Waebrania 3, Kuhani Mkuu. "Sasa Yeye ameketi kwenye mkono wa kuume wa Mungu, Kuhani Mkuu anayeweza kuguswa." Na kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele, ungewezaje kujua ulimgusa Yeye? Angetenda sawa kama Yeye alivyotenda jana. Hiyo ingemfanya Yeye leo. Je! hiyo ni kweli? ["Amina."]

235 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] . . . katika miili migonjwa hapa usiku wa leo. Bwana, Wewe ni Mungu, na hakuna mwingine kama Wewe. Kitu pekee kitupasacho kufanya ni kuamka, tujitikise wenyewe, tumwite Yesu jukwaani. Pia, Baba, wakati Wewe ukija jukwaani, nena kwamba Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele, na jalia tujue usiku wa leo kwamba Wewe ungali ndani ya chombo. Wewe ungali hapa. Ulisema, "Sitakuacha kamwe. Sitakupungukia."

236 Pia jalia ijulikane usiku wa leo, Bwana, kwamba nimesema Kweli. Haijalishi ni maneno mangapi ninapaswa kusema, bado isingekuwa kama Wewe kusema jambo moja. Neno moja tu kutoka Kwako litamaanisha zaidi ya chochote ambacho mwanadamu yeyote angeweza kusema. Tunakuhitaji Wewe, Baba. Njoo jukwaani vya kutosha tu hata watu hawa wanaweza kuona kwamba Wewe uko ndani ya chombo, na ninaamini kwamba kila mwenye dhambi atatubu. Ninaamini kwamba kila aliyerudi nyuma akimbilie madhabahu upesi. Ninaamini kila mtu mgonjwa ataponywa. Si Wewe utatujalia hayo, Bwana?

237 Tunakuita Wewe. Njoo, Yesu. Wengine wataangamia, Bwana. Wengine watakufa kifo cha Milele, kutenganishwa na Mungu, Wewe usipokuja jukwaani. Tunaangamia, Bwana. Baadhi yao wamesahau miujiza Yako mikuu ya uponyaji. Ee Mungu, tembea jukwaani. Tunakuita Wewe. Njoo na uamshe dhamira zetu, Bwana, na Roho wa Kristo ambaye yuko ndani yetu. Tunaomba kupitia Jina la Yesu Kristo.

238 Sasa huku tumeinamisha vichwa vyetu, kama mpiga piano atakuja kwenye piano, ama popote palipo. Na tunaomba kwa ajili ya kicho. Na sasa hebu tuwe tu na kicho jinsi tunavyojua kuwa, kwa muda mfupi. *Amini Tu*, kama utaweza, dada, polepole.

239 Sasa, kila mmoja wenu aombe. Sasa, ombeni wenyewe. Ninataka kujua ni wangapi hapa ndani ambao hawana kadi ya maombi, na wewe ni mgonjwa na unataka Mungu akuguse, naomba mwinue mikono yenu. Vema. Vema. Sasa, ni wangapi walio na kadi za maombi? Inua mkono wako. Vema, kuna karibu maradufu ambao hawana kadi za maombi ya wale walio na kadi za maombi. Bila kujali kama unayo ama huna, hiyo haimaanishi chochote.

240 Hiyo inamaanisha unaita hapa juu. Nilikuwa ninaenda kuwafanya wachungaji washuke, tungeweka mikono juu yenu na kuwaombeni. Sasa, hilo ni—hilo ni jema. Unaona? Hilo

ni jema kabisa. Lakini sikiliza. Unajua, kuwekea mikono, ninaamini hilo. Hiyo ni kweli kabisa. Naam, bwana, jiunganishe mwenyewe na sadaka. Ninaamini hiyo. Bali, tazama, Mrumi wakati mmoja. . . Hiyo ni kanuni ya Kiyahudi. Yairo alisema, "Njoo, uweke mikono Yako juu ya binti yangu naye atakuwa mzima."

241 Bali Mrumi alisema, "Mimi sistahili hata Wewe uje chini ya paa langu. Nena tu neno, mtumishi wangu atapona." Sasa, kama Yeye ni yule yule jana, leo, na hata milele. . .

242 Na mimi sikujui. Mungu Mbinguni anajua kwamba simwoni yeyote isipokuwa huyu dereva wa basi hapa, ambaye ninamjua, kwenye wakati huu. Ninajua nina baadhi ya watu. . . Ndugu Sothmann na hao wako hapa ndani. Mke wangu yuko hapa ndani mahali fulani, lakini si—simwoni kwenye wakati huu. Si—simwoni. Na simwoni Ndugu Sothmann. Lakini hawako hapa. . . Wako hapa, ninamaanisha, lakini sijui ni wapi.

243 Sasa ninawatakeni mwombe. Omba tu kwa unyofu, useme, "Bwana, nisaidie." Na unapoomba, omba maombi ya imani, omba kwamba Mungu atakujalia haja yako. Na useme, "Bwana, ninajua mtu huyo hanijui, lakini kama Wewe utanithibitishia tu kwamba Wewe uko ndani ya chombo, kwamba Wewe upo hapa ndani ya jengo hili usiku wa leo. Basi, ninajua kwamba Ndugu Branham hanijui, hajui chochote kunihusu mimi. Lakini aliniambia, usiku wa leo tu, kwamba Wewe ni yule yule, Wewe ndiye Masihi yule yule, na uliahidi kwamba kama yeye angekuamini Wewe, kwamba Wewe ungefanya kazi zile zile kupitia yeye ambazo—ambazo Wewe ulifanya kupitia Masihi, kwa sababu Roho Wake atakuwa pamoja nasi. Basi kama ninajua, inaweza kuthibitishwa kwamba Wewe upo hapa, basi hayo ndiyo yote yanayonipasa kujua. Nitaamini hilo, kwa moyo wangu wote." Je! utafanya hivyo? Na kama Yeye atatembea jukwaani na kufanya jambo fulani kama Yeye alivyofanya wakati ule, basi utajua ni kazi zile alizofanya Yeye.

244 Angalia kile Yeye alichofanya wakati Yeye alipomwona Petro, Nathanaeli, yule mwanamke kisimani, Bartimayo kipofu, wale ambao walimgusa Yeye, yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu. Unaona? Hivyo ndivyo walivyojua Yeye alikuwa Neno, kwa sababu Yeye aliweza kutambua mawazo yao. Yeye aliahidi, kwenye ishara ya mwisho, kabla ya kuteketezwa dunia, kwamba ingerudi tena, ishara ya mwisho kwa Kanisa. Sisi hapa. Huo hapo ujumbe kwa kanisa la kimadhehebu huko nje. Huu hapa Ujumbe kwa Kanisa, la kipentekoste, Teule, lililovutwa nje. Sasa aminini.

245 Sasa, Baba wa Mbinguni, wako mikononi Mwako. Niko mikononi Mwako. Ninajikabidhi mwenyewe Kwako, ninawakabidhi Kwako, kwamba kazi za Mungu zijulikane, kwamba ujumbe huu mdogo uliokatikakatika usiku wa leo

uweze kudhihirishwa kwa watu hawa hapa Tucson, kote huku chini katikati ya hili jangwa. Baba Mungu, katika kanisa hili dogo lenye upendo, pamoja na maskini mchungaji Wako mwenye upendo hapa, Bwana, kwamba kanisa hili daima litaishi juu ya matokeo ya Neno la Mungu, hata waweze kujua kwamba Yesu angali ndani ya chombo. Kwamba, kwa sababu uamsho hauendelei, hiyo haimaanishi kuwa Yeye ameondoka. Yeye yuko moja kwa moja pamoja nasi, tayari kuitwa wakati wowote, si mgumu kuamshwa, bali atakuja kutuokoa.

246 Ninakuomba Wewe, Bwana, kwamba watu waweze kujua kwamba Wewe ni Mungu, na Wewe ni yule yule jana, leo, na hata milele. Ninajikabidhi mwenyewe Kwako, pamoja na kanisa, kwamba, kati yetu, kati ya imani yao na kipawa ambacho Wewe ulinipa mimi, kwamba imani yao iweze kuitia kazini karama hii ya Mungu, ambayo ingeita kupitia kusanyiko hili, kwamba, watu hawa wasiojulikana, na kufanya kama Wewe ulivyofanya wakati yule mwanamke alipoligusa vazi Lako.

247 Wewe ndiwe Kuhani wetu Mkuu, Bwana. Jalia watu hawa waguse vazi Lako, na Wewe utume Ujumbe Wako kurudi kwao, kama Wewe ulivyofanya kupitia Yesu Kristo, Mwana Wako. Kama sisi, watumishi Wako wasio na faida, tumetakaswa na Damu Yake ya thamani, tuweze kufanya kazi za Mungu zijulikane kwa ulimwengu huu unaokufa katika siku za mwisho. Na sisi tutakusifu Wewe kwa ajili ya hiyo, Baba.

248 Ndipo wakati tutakapoenda nyumbani usiku wa leo, barabarani, tutasema kama wale waliotoka Emau, baada ya Yeye kuwa amekufa, akafufuka, na Yeye akafanya jambo fulani kama Yeye alivyofanya kabla ya Yeye kusulubiwa. Walijua ilikuwa ni Yeye. Hakuna mtu yeyote mwingine angaliweza kufanya hilo. Na ufanye hivyo tena usiku wa leo, Bwana. Fanya kama Wewe ulivyoahidi. Ni ahadi Yako. "Kazi nizifanyazo Mimi yeye atazifanya pia. Nitakuwa pamoja naye, hata ndani yake, hadi mwisho, wa ulimwengu." Itathibitisha hilo, Bwana. Na sisi tutasema mioyo yetu inawaka ndani yetu. Tunaomba katika Jina la Yesu. Amina.

249 Sasa, katika Jina la Bwana Yesu, ninawauliza mketi kimya, kwa kicho, mwamini.

250 Sasa, nikitazama kusanyiko, pamoja na hili Neno la Mungu mbele yangu, ninasema kwamba mtu pekee ninayemtambua hasa ni huyu ndugu *hapa*. Pia sasa ninamwona mke wangu huko nyuma, na nyuma huko. Lakini tuanzie hapa mbele.

251 Sasa wewe omba na useme, "Bwana Yesu, nimesikia mahubiri mengi. Nimesikia vipeo vya mahubiri. Bali ninataka kukuona Wewe, kama wale Wayunani walivyosema, 'Bwana, sisi tunataka kumwona Yesu.'" Hawakutaka kujua filosofia. Walitaka kumwona Yeye, kumjua Yeye, si kitu chochote kingine bali Yeye. Na Yeye ni Neno, unaona, kumjua Yeye binafsi.

Useme, "Mimi ni kama yule mwanamke aliyekuwa anatokwa na damu. Nina haja. Hivi Wewe utajidhihirisha tu Mwenyewe usiku wa leo na kunizungumzia mimi? Wewe ndiwe Kuhani Mkuu. Nisingeweza kujua sauti Yako, labda, kama Wewe ulinena. Lakini kama Wewe ukinena kupitia midomo ya mwanadamu, kama Wewe ulivyosema."

252 Mungu hafanyi chochote bila wakala wa binadamu. Ni wangapi. . .Mnajua hilo. Mnaona? Yeye—Yeye hana budi kumtumia mtu fulani. Sasa hivi mtaninii. . .Kama Yeye atafanya hivyo, na kuthibitisha kwamba Yeye yupo papa hapa pamoja nasi, je! utakubali uponyaji wako? Inua mkono wako, useme, "Nitakubali. Kama ninaweza kumwona Yeye akifanya hivyo, nitaukubali." Mungu awabariki. Sasa omba.

253 Na sasa kama Yeye akifanya chochote kimiujiza, usitie shaka. Amini tu. Unaweza kunitazama, ufanye chochote utakacho kufanya, bali mradi tu unaamini kwamba Yeye yupo. Je! mnaamini hilo, kwa kipawa cha Kiungu, kilichotumwa kutoka kwa Mungu, kikadhihirishwa na Malaika? Na hapa ninasimama, wahudumu hawa karibu nami, papa hapa nje. Hakuna kitu. . .Hiyo ni kweli, ndugu? Sisi sote tumeketi hapa. Haya basi.

254 Sikujui. Mungu anajua hilo. Sijui kitu kimoja kukuhusu wewe, lakini Yeye anajua. Sasa, kupitia Mtu asiyeonekana, Roho Mtakatifu, Yule ambaye anaweza tu kufanya ijulikane kwa madhihirisho Yake, anaweza kukufunulia hasa kile Yeye alichosema Neno litafanya. Wakati Neno likiwekwa katika mwili, ni Mtambuzi wa mawazo ya moyoni. Je! hiyo ni kweli? Hiyo ndiyo sababu Yeye angeweza kufanya hilo. Nyinyi aminini sasa. Iweni na imani. Msitie shaka. Iweni tu na imani.

255 Wakati mzuri kwelikweli! Nafikiri hizi ndizo nyakati za ajabu sana katika maisha yangu, wakati ninapoweza kusimama mbele za kundi la watu na kuwafanya wajue kwamba ibada yao si bure. Dini yoyote nyingine ulimwenguni ni bandia, kando na Ukristo. Dini yoyote nyingine ulimwenguni iko makosani, kando na Ukristo. Ukristo ndiyo pekee ambayo inaweza kukuelekeza kwenye kaburi tupu, na kufungua moyo na kusema, "Yeye anaishi hapa," na kulithibitisha. Sasa, hiki hapa kile Yeye alichoahidi. Je! Yeye atatimiza ahadi Yake? Jambo ndilo hilo. Je! Yeye hutimiza ahadi Yake? Naam, bwana.

256 Unasema, "Vema, Ndugu Branham, shuka chini uniponye."

257 Laiti ningaliweza. Tayari amekuponya. Jambo pekee ambalo Yeye anakutaka ufanye ni kuuamini. Unaona?

"Je! waweza kuniokoa, Ndugu Branham?"

258 Laiti ningaliweza. Lakini Yeye amefanya hivyo tayari. Una. . .Jambo pekee ambalo Yeye angeweza kufanya, kama Yeye alikuwa amesimama hapa amevaa suti hii, ambayo Yeye alinipa, jambo pekee Yeye angeweza kufanya ni kile hasa

tunachomwuliza Yeye afanye sasa, unaona, kutufanya tu tujue kwamba ni Yeye.

259 "Msiogope, ni Mimi. Furahini." Unaona? Wanafunzi, wakati Yeye alipokuwa anatembea juu ya maji, walidhani ilikuwa ni roho, mzuka, ama kitu fulani. Waliogopa. Akasema, "Msiogope. Ni Mimi" Unaona? Na hicho ndicho Yeye angesema usiku wa leo, "Msiogope. Ni Mimi."

260 Ninamwangalia mwanamke aliyeketi tu hapa, akinitazama moja kwa moja. Na kama mnaweza kuona Hiyo sasa, ile pale Nuru ile juu ya mwanamke aliyeketi papa hapa. Sikujui. Bali, hiki hapa kitu kimoja, unasumbuliwa na tatizo kwenye mgongo wako. Je! hiyo ni kweli? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Imani yako inakuponya.

261 Niambieni kile alichogusa. Sijawahi kumwona maishani mwangu. Je! sisi ni wageni mmoja kwa mwenzake? Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Kwa hiyo, mnaona, sijawahi kumwona mwanamke huyo maishani mwangu. Ila nilimwona namna *hii*, na nikajua hapa ndipo ilipokuwa. Vema. Naam.

262 Hapa, hapa pana kitu. Huyu hapa msichana mdogo aliyeketi hapa kwenye kiti cha mbele, mtoto tu. Punde tu nilipotaja jina lake, a—alianza kulia. Maskini msichana huyu anatafuta kitu fulani halisi. Dada yake analia, nyuma yake. Simjui mtoto huyu, sijawahi kumwona maishani mwangu, kama nijuavyo. Lakini anatafuta ubatizo wa Roho Mtakatifu. Hiyo ni kweli. Je! hiyo ni kweli, msichana mdogo? Hiyo ni kweli. Inua maskini mkono wako. Unaona? Haya basi. Hatoki hapa. Anatoka mashariki mwa hapa. Yeye ni binti ya mhudumu mmishenari. Jambo jingine, baba yake anatamani kuniona kuhusu swali fulani. Sijawahi kumwona maishani mwangu, bali hiyo ndiyo kweli hasa. Usiogope, mpenzi. Utapokea Roho Mtakatifu. Imani yako inaifanya. Amini tu.

263 Ikiwa mtoto huyo mdogo anaweza kufanya hilo. . . Mwulize mtoto huyo, uone kama ni sahihi au si sahihi. Kama maskini mtoto huyo. . . Waligusa kitu gani? Msichana mdogo, una kadi ya maombi, mpenzi? Huna? Hu—huihitaji. Unaona? Una zaidi ya kile kadi ya maombi ilicho, mpenzi. Unayo imani.

264 Kumbukeni, atapokea Roho Mtakatifu. Yeye, atapokea huyo. Kwa kweli, Huyo yuko moja kwa moja karibu naye sasa. Unasema, "Unajuaje?" Nilijuaje kilichokuwa shida, kile alichokuwa anataka? Unaona? Sasa, ikiwa mtoto huyo, "mtoto atawaongoza," kwa nini si wewe sasa?

265 Yupo mama anayeketi moja kwa moja hapa, akinitazama. Anaugua hali ya wasiwasi. Anaomba kwa ajili ya mume wake, pia, ambaye hajaokoka. Utaamini kwa moyo wako wote, unaweza kupokea kile ambacho umeomba. Amina.

266 Hapa, msichana aliyeketi moja kwa moja *hapa* nyuma katika safu ya nje, ana tatizo la kike. Wewe amini kwa moyo wako wote, utapona. Unaamini hilo?

267 Yupo mama mweusi aliyeketi moja kwa moja nyuma yake pale. Yuko katika maombi, lakini anamwombea mpendwa. Ni mwanaume mkongwe, baba mkwe. Na huyo baba mkwe amekuwa mgonjwa kwa miaka. Hiyo ni kweli. Mimi ni mgeni kwako. Je! hiyo ni kweli? Hilo lilisababishwa na namna fulani ya ajali ambayo ilianzisha tatizo hilo. Kama hiyo ni kweli, inua mkono wako. Vema. Unaamini? Unaweza kupokea kile ulichoomba.

268 Kwa kweli hiyo imeanza kuzunguka. Mama mwingine mweusi anayeketi moja kwa moja huko nyuma, anaugua ugonjwa wa pumu. Mama huyo anaenda kuukosa. Mungu, nisaidie. Bibi Jamison, wewe amini kwa moyo wako wote. Simama kwa miguu yako. Sikujui. Lakini, wewe amini kwa moyo wako wote.

269 Unasema, "Kujua jina lake?" Mbona, hakika. Je! Yeye hakumwambia Petro kile jina lake lilikuwa? Naam. Hakika. Yeye anajua mambo yote.

270 Huyu hapa mwanamume ameketi hapa, anaenda kufa kwa kansa, kama kuna kitu hakitamgusa upesi sana. Ana kansa. Hiyo ni kweli. Unaamini? Unaamini? Unaamini Mungu anaweza kuniambia kuwa wewe ni nani? Bw. Ladd, basi, kama unaamini kwa moyo wako wote, unaweza kuponywa. Sijawahi kumwona mtu huyo maishani mwangu.

271 Mwiteni Yesu. Yuko miongoni mwenu sasa. Hivi hamwoni? Je! mnaamini? Iweni na imani katika Mungu. Je! mnaamini kwamba mnaweza kumwamsha Yeye katika dhamiri yenu sasa? Mnaona? Je! mnaamini? Kama mnaamini, wekeni mikono yenu mmoja juu ya mwenzake, namna *hii*. Wekeni tu mikono yenu kila mmoja juu ya mwenzake. Mwiteni jukwaani. Huyo ni Yeye. Je! mnaamini hilo? Huyo ni Yeye. Waulizeni watu hawa. Sijawahi kuwaona maishani mwangu.

272 Sasa iko kila mahali, kote katika jengo sasa, mkiwa mmewekeana mikono kila mmoja na mwenzake. Hivi hamwezi kuchukua neno langu? Kama Mungu amethibitisha kwamba nimewaambia kweli, mnaona, basi chukueni neno langu kwa ajili yake. Ninawaambieni kilicho kweli. Kweli ni nini? Wekeaneni mikono mmoja na mwenzake. Msitie shaka. Biblia ilisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, watapata afya." Huyu hapa Yesu miongoni mwetu, sasa hivi, Roho wa Kristo.

273 Sasa, unapoweka mikono yako juu ya mtu huyo aliye pamoja nawe, sasa wewe waombee. Endelea tu, weka mikono yako juu yao na uombe. Ninaenda kuomba kutoka hapa. Na ninaamini

Mungu anaenda kuponya kila mmoja wenu. Wewe weka mikono yako juu yao, na uamini, wakati tukiomba.

274 Bwana Yesu, tunakushukuru Wewe. Moyo wangu unapiga mbio, kwa kuwa Wewe huyu hapa, papa hapa Tucson. Wewe huyu hapa, moja kwa moja hapa katika kusanyiko hili la kanisa. Upo hapa miongoni mwa watu hawa. Umethibitisha hilo, Bwana. Mambo haya yangewezaje kufanywa isipokuwa yawe ni ya Mungu? Si ajabu mtume alisema, "Mtu aliyethibitishwa na Mungu miongoni mwetu, kwa ishara na maajabu, ambayo (Yeye) Mungu alifanya kupitia Yeye miongoni mwetu sote, ambao sisi ni mashahidi." Na huyu hapa Mtu yuyo huyo, Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, katika umbo la Roho Mtakatifu, usiku wa leo, akitembea miongoni mwetu, akithibitisha Maneno Yake. "Kazi nizifanyazo mimi mtazifanya pia." Tunajua kwamba Wewe upo hapa, Bwana. Hujatuacha.

275 Sasa, watu hawa wamewekeana mikono kila mmoja na mwenzake. Wao ni waaminio. Wanaombeana mmoja na mwenzake, na wanaamini kwamba Wewe unaenda kuwafanya wazima.

276 Kwa Neno la Mungu aliye hai, kwa changamoto ambayo Neno linatoa, kwamba, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio." Katika Uwepo wa Yesu Kristo aliyefufuka, Mwana wa Mungu, katika Uwepo Wake! Uwepo, Roho Mtakatifu ambaye hivi sasa yupo hapa, na amethibitisha kwamba ni Yesu miongoni mwetu, ametuamsha, Bwana, kutoka kwa usingizi wetu, hata mioyo yetu inadunda upesi kwa imani na sifa.

277 Katika Jina la Yesu Kristo, naomba kila ugonjwa ufunguke kutoka kwa watu hawa kwenye dakika hii. Jalia wawekwe huru kutokana na ugonjwa wao wote na mateso waliyo nayo. Ninamwamuru Shetani, kwa Uwepo wa Yesu Kristo, katika ukumbusho wa Neno Lake, lililosema, "Katika Jina Langu watatoa pepo." Sisi, kama wanaume na wanawake waaminio, tunampinga ibilisi huyu. Katika Jina la Yesu Kristo, liache kusanyiko hili. Toka ndani ya kila mmoja wao. Pia ninaomba waondoke wakiwa huru, usiku wa leo, kuenda nyumbani, kujikuta wenyewe wakiwa huru kutokana na ugonjwa, huru kutokana na maumivu, huru kutokana na mateso, kila mmoja wao, Bwana. Katika Jina la Yesu Kristo naomba iwe hivyo.

278 Huku vichwa vyenu vimeinamishwa sasa, endeleeni kuombeana mmoja na mwenzake. Sasa, kama kuna mwanamume au mwanamke, ambao wamekuwa na shaka moyoni mwao, mvulana au msichana, na anaamini kwamba upo sasa Uweponi mwa Yule ambaye nimenena kumhusu usiku wa leo, Yule ambaye ametenda kikamilifu na kukuambia; na kukuthibitishia kwa Neno Lake, kwamba Yeye angefanya hivyo, na amekuja na kufanya hasa kile Yeye alichosema Yeye angefanya, unaona, miongoni mwetu usiku wa leo. Na kama

wewe si mtoto wa Mungu, hivi utatembea kuja hapa juu kwenye madhabahu huku Roho Mtakatifu ananitia upako na kuwatia upako hawa wengine, na kuturuhusu tukuombee? Naomba uje wakati tumeinamisha vichwa vyetu, tuinamishe tu vichwa vyetu kwa dakika moja, tunapovumisha kimoyomoyo, "Amini tu, mambo yote."

279 Unasema, "Ndugu Branham, nimetafuta Mungu kwa miaka, na si—si—sijaweza kamwe kujazwa na Roho. Mimi si Mkristo aliyezaliwa mara ya pili. Ni—ninataka nizaliwe tena. Ni—ninaitaka kabisa. Na mimi, Ndugu Branham, ninataka uniombee."

280 Hivi utakuja hapa juu na kusimama hapa, huku tukivumisha huu kote, ama kuuimba mara moja, huku vichwa vyetu vimeinamishwa na mioyo yetu kuinamishwa? *Amini Tu*. Ninajisikia kuongozwa kufanya hili, kwa njia fulani. Sijui. Huwa sifanyi hili. Bali ninajisikia kuongozwa kulifanya sasa hivi, kwamba wito huu ufanywe. Ili, kwamba, kwenye mwisho wa wakati, nitakaposimama mbele zenu tena . . . Labda nisiwahi kusimama tena, kama nikirudi hapa mwaka mmoja kuanzia leo, kutakuwa na . . . Kama nikiishi kumaliza mwaka, wengi hapa hawatamaliza. Mnaona? Hawatakuwepo, maana wapo watu wakongwe hapa. Na—na wengi wenu hawatakuwa hapa mwaka mmoja kuanzia usiku wa leo, bali itabidi nikutane nanyi wakati fulani. Kwa hiyo, katika Uwepo wa Kristo, ninawaulizeni mje mbele sasa, katika Jina la Yesu, na kumkubali Yeye kama Mwokozi wako, huku tukiimba sasa na vichwa vyetu vimeinamishwa.

> Amini tu, ninii tu . . .

Unataka niombe pamoja na wewe, hivi utakuja hapa?

> Mambo yote yawezekana, hivi wewe hutaninii tu . . .

281 Amini tu Yeye yupo hapa, wazia tu, Yule mpendwa ambaye itakubidi kusimama katika hukumu Yake wakati fulani. Kama dhambi inakusumbua, mbona usije mbele?

> . . . amini tu,
> Yote . . .

Hiyo ni kweli. Njoo moja kwa moja huku juu. Nyi' nyote ni . . . Njoo papa hapa, dada. Mtu mwingine aje moja kwa moja sasa? Njoo moja kwa moja mbele.

> Ee Bwana, mimi . . .

Jambo ndilo hilo. Jambo ndilo hilo. Njoo.

> . . . Bwana, nitaamini,

282 "Nitaamini hivi sasa, Bwana, Wewe upo hapa."

> Yote . . .

"Nimejaribu, Bwana, bali sijui. Mambo yote yanawezekana. Bwana, naamini. Ninataka kuwa sahihi na Mungu. Ningeninii . . ." Mungu awabariki nyinyi, wavulana, mnaokuja kutoka nje.

283 [Ndugu fulani anasema, "Unawataka waingie *hapa* ndani?"—Mh.] (Sasa, hiyo ni sawa, ndugu. Ni sawa tu. Nitateremka moja kwa moja niende kwao. Nitawapelekeni nyote chini . . .?. . .)

. . . Ee Bwana, naamini,
Mambo yote yawezekana, Ee Bwana, na . . .

284 Bwana, baada ya Wewe kufufuka kutoka kwa wafu, miaka elfu moja mia tisa iliyopita, na hapa Wewe ulitoa ahadi kwamba sisi tungekuona Wewe katika siku za mwisho, kwamba Wewe ungefanya jambo lili hili. Na hapa Wewe unakuja, usiku wa leo, moja kwa moja mbele ya macho yangu, katika wakati huu wa elimu, wakati wa sayansi, na kuvunja kila sheria ya sayansi, kuvunja kila kitu ambacho wapinzani wamesema, na kushuka moja kwa moja miongoni mwetu, na kuthibitisha kwamba Wewe umefufuka kutoka kwa wafu. "Nitaamini, Bwana. Ninaamini," huku tukiuimba mara nyingine tena.

Bwana, naamini . . .

285 Hivi mtakuja sasa, nyinyi wengine? Njoni moja kwa moja. Pandeni juu, nyinyi nyote. Wote wanaotaka kumkubali Kristo usiku wa leo, mbona msije?

. . . mambo yawezekana, Ee Bwana, naamini;
Ee Bwana . . . ("Bwana, nitaamini.")

286 Hakuna chochote kingine kipasacho kufanywa, Bwana. Hiyo ndiyo ishara ya mwisho uliyoahidi Wewe. Kuhubiri Neno, kuponya wagonjwa; kumbukeni, Neno limeshahubiriwa, wagonjwa wameishaponywa. Lakini hii hapa ishara ya mwisho kwa Kanisa lililoitwa litoke, Kanisa la Kipentekoste lililoitwa litoke. Ishara yake ya mwisho. "Nitaamini."

287 Sasa, kama ambavyo tumepata hawa, idadi kamilifu hapa usiku wa leo, ya saba, inamaanisha ukamilifu. Nilitaka tu kuwa na hakika. Roho Mtakatifu . . . Hamnioni kamwe nikiwa na ibada ya uponyaji, halafu nigeuke moja kwa moja kurudi nyuma na kufanya wito wa madhabahuni. Mnaona? Bali Roho Mtakatifu alisema, "Lifanye." Mnaona? "Lifanye sasa hivi. Huu ndio wakati. Wewe lifanye." Niliwaza . . . Nilimgeukia Ndugu Mack. Akasema, "Wewe lifanye." Hawa hapa, saba, idadi kamili. Labda wito wao wa mwisho, ila wameitikia. Wamefanya hasa kile ambacho Mungu aliwaambia wafanye.

288 "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu na kumwamini Yeye aliyenipeleka Mimi, yu na Uzima usio na mwisho, hataingia Hukumuni, bali amepita kutoka mautini kuingia Uzimani." Walipita kutoka mautini kuingia Uzimani.

289 "Yeye anayenionea aibu Mimi mbele za wanadamu, huyo nitamwonea aibu mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu. Lakini yeye atakayenikiri Mimi mbele za watu, huyo nitamkiri mbele za Baba Yangu na Malaika watakatifu." Hawa hapa wamesimama, wanaume watatu na wanawake wanne.

290 Na hivi mlijua kwamba hivyo ndivyo viwango vya uzazi vilivyo ulimwenguni leo, katika Marekani? Wanawake wanne kwa kila wanaume watatu. Hivyo ndivyo viwango vya uzazi vilivyo. Hivi hapa viwango vya uzazi tena usiku wa leo, vikirudi ndani ya kanisa. Marekani inapata yake ya mwisho. Imekwisha. Hayo tu. Tuko kwenye wakati wa mwisho.

291 Sasa sijui kama wanawake fulani, mama fulani mzuri au mwanamke hapa, ambaye amejazwa na Roho Mtakatifu, watatu au wanne wenu, wangekuja hapa, wasimame pamoja na dada hawa, wakati ninapoenda kuwaombea. Na ndugu watatu au wanne, labda ndugu zetu wahudumu hapa, washuke chini, wasimame karibu na hawa vijana wazuri wa kiume waliosimama hapa, wasimame hapa wakati tunapoweza kushuhudia pamoja. Ninaenda kushuka chini, niombe, na kuweka mikono juu ya watu hawa. Na ninataka kila mtu ndani ya kanisa hili aamini pamoja nami, wakati tukiomba. Hiyo ni kweli. Mungu awabariki, ndugu. Ninashuka chini pamoja nanyi, kuweka mikono juu yao.

292 Sasa ninataka kila mtu awe na kicho kabisa, kama mtaweza, kwa muda mfupi tu, sehemu yenye kicho kuliko zote.

293 Sasa tazameni. Haya ndiyo yote wawezayo kufanya. Ni. . . Angalia. Mnajua, walisikia Sauti ya Mungu, nao wametembea kuja hapa juu. Hawa vijana wanaume katika wakati huu, wanawake hawa katika wakati huu, walitembea kuja hapa juu kufanya maungamo ya hadharani, wamemalizana na dhambi. Nilisema, "Yeyote anayetaka kumpokea Yesu Kristo kama Mwokozi wao, njoo mbele."

294 Na Uwepo wa Mungu ukitambua mawazo, ukiwaambia watu kilicho shida yao, kuwa wao ni kina nani, kinachowahusu, mahali wanapotoka, unaona, kama huyo si Kristo, basi ni kitu gani? Ni ahadi. Mungu alisema Yeye angelifanya. Basi watu hao, labda mara ya kwanza wamewahi. . .Na hao, wenye dhambi, walisema, "Ndiyo, ninaamini hilo. Jambo ndilo hilo. Hilo hapo Neno lililofanyika—lililodhihirishwa. Limefanyika mwili. Neno limekuwa mwili tena, Mungu akifanya kazi kupitia mwili wa mwanadamu. Tunajua ni kweli." Ndipo wakainuka na kusema, "Nimemalizana na dhambi." Hayo ni maungamo ya hadharani. Hayo hutimiza hilo.

295 Sasa, enyi watu wapendwa ambao mmekuja hapa juu, siku moja inanibidi kukutana na nyinyi, dada, upande wa pili wa mpaka huko ng'ambo, kila mmoja wenu. Sina budi kukutana nanyi huko. Sina budi kutoa hesabu kwa kile ambacho

nimesema. Ndugu, inanibidi kutoa hesabu. Wewe, huenda umefanya mambo makubwa mazuri. Huenda umewatii wazazi wako. Huenda umefanya mambo ya ajabu. Bali jambo kubwa kuliko yote uliyofanya maishani mwako ni lile unalofanya sasa hivi. Unaona? Hilo ndilo jambo kubwa kuliko yote uliyowahi kufanya.

296 Sasa, kama Mungu—kama Mungu ametuma Roho Wake chini na amethibitisha, na halafu Kitu kile kile kikanena kupitia mimi na kusema, "Fanya wito." Sasa, ikiwa umewahi kuwa katika mikutano hapo kabla, unajua sifanyi hivyo. Nitaugeuza kwa mchungaji. Lakini Yeye alisema, "Wewe fanya hivi." Mnaona? Ndipo mimi nikafanya. Upesi sana, nilikuwa ninaenda kufanya. Kulikuwa na mtu fulani hapa, na ilikuwa mahali fulani niliona Nuru ile ikisonga juu yao. Nikaanza. Ndipo mara moja, Hiyo ikakatiza. Je! mlitambua vile Hiyo ilibadilika? Kasema, "Wewe fanya hili." Kasema, "Ita sasa hivi." Hayo ndiyo yote niliyoweza kufanya. Kweli. Ndiyo yote niliyoweza kufanya. Nyinyi hapa.

297 Sasa, Yesu alisema, katika Yohana Mtakatifu 5:24, unaona, ni hili, kwamba, "Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka Mimi, yu na Uzima usio na mwisho." Unaamini hilo, mwanangu? Mnaamini hilo, kila mmoja wenu enyi wanaume? Enyi wanawake mnaamini hilo? Hayo ndiyo yote mliyoweza kufanya.

298 Ndipo mnafanya nini? Kubalini. Hakuna kitu mwezacho kufanya. Sema, "Bwana," moyoni mwako, "ninasikitika kwa ajili ya kile nilichofanya. Kwa furaha ninakubali kile Yesu alichonifanyia. Usiku wa leo, tangu wakati huu na kuendelea, ninaenda kuishi kwa ajili Yake. Ninaenda kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wangu. Ninaenda kukubali ubatizo wa Kikristo. Ninaamini kwamba Wewe utanijaza na Roho Mtakatifu. Ninataka kukuishia Wewe."

299 Kitambo kidogo tu na utakuta kila kitu kimebadilika, na wewe ni kiumbe kipya. Uhai mpya huingia, nawe unaishi kuanzia hapo na kuendelea. Na mimi nitakutana nanyi tena kwenye kiti cha hukumu cha Kristo, kila mmoja wenu. Nitakutana nanyi kule, nami nitawajibikia kile mimi . . . Mungu ataniwajibisha. Lakini ikiwa mtalikubali juu ya . . . Useme, "Chochote nilichofanya, Wewe wajua, nilitembea kuja hapa juu mbele za watu hawa kuonyesha kwamba ninasikitika. Sininii . . . Sikumaanisha kufanya hivyo. Sitaki kulifanya tena. Nimemaliza." Hilo ndilo . . .

300 Sasa ninawatakeni mwinamishe vichwa vyenu. Ninataka kila mmoja wenu ndugu na dada mweke mikono yenu juu yangu. Ninataka kila mtu wa kanisa hapa ndani, kila Mkristo, kuinamisha vichwa vyenu katika maombi manyenyekevu wakati ninapoomba. Na je! mtaomba pamoja na mimi, kwamba Mungu ajalie haja hii?

301 Sasa, Baba wa Mbinguni, hapa amesimama mwanamke akilia, msichana, msichana mrembo amesimama hapa, akilia. Yeye. . . [Ndugu Branham anaendelea kuomba pamoja na watu. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

302 . . . juu ya Wewe kuthibitisha kile Wewe ulichosema Wewe ungefanya. Uliahidi kwamba Wewe ungefanya hivyo. Ulishuka chini na kuponya wagonjwa na wanaofariki, nao wamebadilishwa kutoka mautini kuelekea Uzimani.

303 Na ndipo wengine, wanaokufa kiroho, walikuja madhabahuni mbio. Malaika wa Mbinguni wanafurahi, kulingana na Neno la Mungu, "Mpotevu amerudi." Yesu alitoa pepo kwa kidole cha Mungu, bali wakati Yeye alipomwokoa kondoo, Yeye alimweka juu ya bega Lake, sehemu yenye nguvu kuliko zote ya mwili Wake, na kumleta ndani.

304 Sasa hawa hapa, Bwana. Hawa ni Wako. Ninawakabidhi Kwako, kama ishara za upendo wa Uwepo Wako usiku wa leo. Wadumishe, Bwana, katika amani kamilifu. Na uwape Uzima wa Milele, ili wasiangamie kamwe, bali waishi milele. Mungu, Wewe uliahidi kwamba Wewe ungemfufua katika siku ya mwisho. Ninaamini hilo. Na hao ni Wako.

305 Sasa huku tumeinamisha vichwa vyetu, kila mmoja. Ninataka kuwaulizeni ambao mmekuja madhabahuni sasa hivi, kwamba, kutoka—kutoka kilindi cha moyo wako, wewe njoo katika unyofu. Na kutoka kwenye kilindi cha moyo wako wewe amini kwamba Biblia ni sahihi; kwamba Yesu Kristo, Mwana wa Mungu, alikufa badala yako. Wewe hustahili hiyo. Wewe hustahili. Unajua hilo. Lakini kwa sababu kwamba hukustahili, Mungu alimtuma Yeye, Yule aliyestahili; ili wewe, katika kutokustahili kwako, mweze kufanywa wana na binti za Mungu. Hakuna kitu. . . Ila tu kitu fulani moyoni mwako kinakuambia kwamba hilo ni kweli, na unalikubali. Unaamini Hilo kwa moyo wako wote, na kumkubali Yeye kama Mwokozi wako. Si chochote ulichofanya, bali kile umeamini kwamba Yeye amefanya. Unaamini Hilo. Ninataka uinue mkono wako, useme, "Mimi sasa, katika Jina la Kristo, nitamkubali Yesu Kristo achukue mahali pangu huko." Hayo ndiyo yote Yeye anayotaka kufanya, kuchukua mahali pako. Mungu akubariki wewe, na akubariki wewe. "Atachukua mahali pangu."

306 Sasa ninataka mgeuke moja kwa moja kwenye kusanyiko, moja kwa moja kuelekea kusanyiko. Geukeni moja kwa moja namna *hii*, kuelekea wasikilizaji. Ninawatakeni enyi watu mnaosimama, mkiomba, ninawatakeni nyote kuwatazama watu hawa. Sasa waangalieni wanapoinua mikono yao.

307 Nyinyi mnaojua kwamba mlikuwa ni wenye dhambi, na sasa mmepita kutoka mautini kuingia Uzimani, inueni mikono yenu juu hewani tena namna *hiyo*. Inueni mikono yenu. Ninawatakeni

nyinyi kwenye wasikilizaji mnaowakubali kama ndugu zenu na dada, inueni mikono yenu namna *hiyo*. Sasa, nyinyi hapo.

308 Utukufu kwa Mungu! Sifa kwa Mungu! Wao ni Wako. Hao ni wana na binti za Mungu, waliokombolewa.

309 Sasa hebu, kila mtu tuinamishe, vichwa vyetu, na kutoa shukrani kwa Mungu kwa ajili ya kile Yeye amewafanyia.

310 Ni wangapi hapa ndani, ambao walikuwa wagonjwa, mlijihisi wagonjwa, na sasa wewe inua mkono wako, useme, "Ninaamini kwamba ninajua kwamba Uwepo wa Yesu Kristo usiku wa leo umenifanya mzima. Mimi si mgonjwa tena." Inueni mikono yenu, kila mmoja. Angalieni hapa, kusanyiko lote. Vema. "Mimi sasa ni mzima kwa Damu ya Yesu Kristo."

311 Sasa, hebu tuinamishe vichwa vyetu tena. Basi kila mmoja, enyi watu, pandeni juu, wekeni mikono yenu juu ya watu hawa, enyi Wakristo. Mnataka kuwapatia mkono wa ushirika, na kuwabariki, na kuwaalika kwenye kanisa lenu, au chochote mnachofanya. Mungu awe pamoja nanyi.

312 Basi hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa. Na kila mmoja wetu, katika njia yetu wenyewe, tumpe Mungu shukrani kwa yale ambayo Yeye amefanya. Vema. Hebu tuinamishe vichwa vyetu.

313 Ndugu Mack, mbona usije hapa na kutuongoza katika maombi haya. Naam, Bwana. Naam.

63-1103 Nenda, Kamwamshe Yesu
Grantway Assembly Of God
Tucson, Arizona Marekani

SWAHILI

©2020 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:



VOICE OF GOD RECORDINGS

P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.

www.branham.org